




**Katibu** Mkuu CCM awaweka kitimoto mawaziri

UKURASA 3




UKURASA 11


# Nipashe

Jumatatu Februari 6, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581213

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital | nipasheTZ | nipasheTZ | nipasheTZ | 0745 700710

LIKE & FOLLOW US


KASI YA SARATANI

# Uchunguzi maji ya maiti kuhifadhi samaki waanza

• **Sampuli** 14,000 zakusanywa, wanawake waongoza kuugua saratani nchini...*Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

### CRDB YAKABIDHI KITUO CHA MAWASILIANO OCEAN ROAD

BENKI ya CRDB imekabidhi kituo cha mawasiliano kwenye Taasisi ya Saratani ya Ocean Road (ORCI) ikiwa ni matokeo ya fedha zilizokusanywa katika mbio za...

UKURASA WA 7

### MIILI YA AJALI NA KESI ZA POLISI YAIGHARIMU MUHIMBILI MAMILIONI

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH), imesema kwamba kati ya changamoto inayokumbana nayo ni pamoja na kutoa misamaha, kugharamia huduma...

UKURASA WA 17

### MUFTI ZANZIBAR AWATAKA WAZAZI KUKEMEA USHOGA

OFISI ya Mufti ya Zanzibar imewataka wazazi kukemea uhamasishaji wa matukio ya ushoga ambayo yanakwenda kinyume...

## Waliochelewa kufika katika ajali iliyoua 20 matatani

UKURASA 4



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla (wa pili kushoto) na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, wakizindua rasmi kituo cha mawasiliano kwenye Taasisi ya Saratani Ocean Road jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Kituo hicho kilijengwa kwa ufadhili wa Benki ya CRDB kwa kutumia fedha zilizokusanywa katika mbio za CRDB Bank Marathon 2021. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Adaiwa kuua dada wa kufikia, akamchoma kisu mama ubavuni

UK. 4

**MICHEZO** **SIMBA SC, AL HILAL KUMENOGA CAF** UK.24 **KATUNI** UK.6



Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Ujenzi), Balozi Mhandisi Aisha Amour, akifafanua jambo kwa wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali wakati kamati hiyo ilipotembelea Ofisi za Bodi ya Mfuko wa Barabara jijini Dodoma kwa ajili ya kujifunza utendaji kazi wa bodi hiyo, (kushoto kwake) ni Mwenyekiti wa kamati, Naghenjwa Kaboyoka na Meneja wa Mfuko wa Barabara, Eliud Nyauhenga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Uchunguzi maji ya maiti kuhifadhi samaki waanza

**Na Vitus Audax,** MWANZA

HOSPITALI ya Rufani ya Kanda ya Bugando imeanza uchunguzi kubaini ukweli wa taarifa za maji ya kuhifadhi maiti kutumika kuhifadhi samaki.

Uchunguzi huo wa kisayansi unafanywa kufuatia agizo la Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango la kufanya utafiti kuhusu kinachodaiwa kuwapo ongezeko la magonjwa ya saratani mikoa ya Kanda ya Ziwa linalosababishwa na matumizi ya maji hayo kuhifadhi kitoweo hicho kinachotumiwa na wakazi wengi wa mikoa hiyo.

Utafiti huo unafanyika kupitia sampuli mbalimbali za wagonjwa wa saratani pamoja na wale wasiokuwa na ugonjwa huo wanaoishi Kanda ya Ziwa ili kubaini ukweli wa madai hayo kama alivyoamuru Makamu wa Rais wakati wa uzinduzi wa wodi ya wagonjwa wa saratani hospitalini huko hivi karibuni.

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Saratani na Mkuu wa Idara ya Saratani wa hospitali hiyo, Dk. Nestory Masalu, alibainisha hayo mwishoni mwa wiki wakati wa maadhimisho ya Siku ya Saratani Duniani.

Bingwa huyo wa saratani alisema utafiti wao huo unatarajiwa kuchukua muda wa miezi sita.

"Tayari tumekusanya sampuli 7,000 za watu wenye saratani mbalimbali pamoja na sampuli 7,000 za watu wasiokuwa na saratani, wote wakiwa na umri uleule na wanaishi mazingira hayo hayo ili tujue sababu za hawa kupata ugonjwa huo na wengine kutokupata ugonjwa huo," alisema Dk. Masalu.

Alisema kwa sasa tayari wana taarifa hizo na wanafanya uchambuzi wa taarifa hizo na majibu yake yanatarajiwa kutolewa baada ya miezi sita kutokana na ugonjwa huo kuchukua muda mrefu kuleta majibu sahihi.

Dk. Masalu alibainisha kuwa kwenye hospitali hiyo kwa sasa wanapokea wagonjwa wa saratani takriban 1,500 kwa mwaka, idadi inayoonekana kuwa kubwa zaidi tangu kuanzishwa kwa huduma hiyo mwaka 2009.

Alisema kuwa tangu kuanza kutolewa kwa huduma hiyo hospitalini huko, wamefanikiwa kutoa huduma kwa wagonjwa wa saratani 55,000 huku wagonjwa 10,000 wakifariki dunia wakati wa matibabu.

"Ninatoa wito kwa wananchi hasa wale wenye umri mkubwa kuwa na utaratibu wa kupima afya zao mara kwa mara ili kukabiliana na ugonjwa huo mapema," alisema Dk. Masalu.

Baadhi ya mashuhuda waliopona ugonjwa wa saratani, waliungana na bingwa huyo kuwashauri wananchi kuwa na utaratibu wa kupima afya zao mara kwa mara ili kukabiliana na ugonjwa huo mapema pindi wanapogundulika.

"Nimefanyiwa upasuaji wa titi kutokana na ugonjwa huu na mpaka sasa hali yangu ni nzuri. Ninashukuru Mungu ugonjwa huu umepona.

"Kikubwa ni kuhakikisha unapima mapema ili kuepusha kukaa na ugonjwa huu ukafikia hatua ngumu kutibiwa," alisema Geredina Nzogela.

Katika maadhimisho hayo, Hospitali ya Rufani ya Kanda Bugando ilitoa huduma za upimaji wa magonjwa ya saratani ya shingo ya kizazi, saratani ya tezi dume na saratani ya matiti bila malipo.

Kwa muda mrefu kumekuwa na madai mengi kuhusu kasi ya ongezeko la saratani Kanda ya Ziwa, baadhi wakijihusisha na kemikali zinazotokana na migodi mingi iliyoko kwenye ukanda huo pamoja na kemikali zinazotumika kwenye kilimo cha pamba, tumbaku na kahawa.

# Wanawake nchini waongoza kwa kuugua saratani

**Na Elizabeth Zaya**

MKURUGENZI Mtendaji wa Taasisi ya Saratani Ocean Road (ORCI), Dk. Julius Mwaiselage, amesema ugonjwa wa saratani nchini unaendelea kuongezeka kwa kasi huku wanawake wakiongoza kwa kuugua kwa asilimia 70.

Akizungumza mwishoni mwa wiki wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Saratani Duniani yaliyofanyika Dar es Salaam, Dk. Mwaiselage (pichani) alisema saratani inayoongoza kwa sasa ni ya mlango wa kizazi, ikichukua asilimia 35 ikifuatwa na ya matiti asilimia 15.

"Unaweza kuona wanawake ndio waathirika zaidi kuliko makundi mengine yoyote kwa sababu hizo zote mbili waathirika ni wanawake," alisema Dk. Mwaiselage.

Alitaja saratani inayoshika nafasi ya tatu kuwa ni ya koo la chakula, ya nne ni ya ngozi na ya tano ni ya muunganiko.

"Hii saratani ya muunganiko ni ile ya mdomoni, shingoni na kichwani," alifafanua Dk. Mwaiselage.



Saratani inayoshika nafasi ya sita kwa sasa ni ya tezi dume, kiongozi huyo wa ORCI akisema: "Kwa hiyo, kubwa katika ujumbe wa mwaka huu ni kwamba saratani inaongezeka sana nchini, hivyo ningependa kuwaasa wananchi wafike kuchunguza afya zao mapema kwa sababu ikigundulika mapema inatibika na kupona.

"Tunamshukuru sana Rais Samia Suluhu Hassan ameboresha sana huduma za saratani nchini, zimesambaa katika hospitali zote za kanda, lakini hapa Ocean Road kwa sasa tuna mashine za kisasa za tiba za uchunguzi na upatikanaji wa dawa ni asilimia 100."

Alisema asilimia kubwa ya wagonjwa wa saratani hufika hospitalini kutibiwa wakati tayari ugonjwa umefika katika hatua ya juu zaidi na hivyo kusababisha wengi wao kufariki dunia.

Alisema tayari taasisi hiyo imezindua kituo cha mawasiliano ya ugonjwa huo ambacho lengo lake kubwa ni kurahisisha mawasiliano kati ya wananchi, wagonjwa, ndugu zao na wataalamu wa afya.

"Kwa sasa watu watakuwa wanapiga simu moja kwa moja kufahamu au kuuliza maswali kuhusiana na jambo lolote linalohusiana na ugonjwa huo wa saratani.

Pia alisema taasisi hiyo inakamilisha mradi mkubwa unaojulikana kama PET/CT Scan ambao utahusisha kufunga kifaa maalum cha kuchunguza saratani katika hatua ya chembechembe hata kabla ya uvimbe itakayoanza kutumika Machi mwaka huu.

Dk. Mwaiselage alisema mashine hiyo ni ya kipekee ambayo hupatikana katika nchi za Ulaya na Marekani, nchi za Asia pekee ambako Watanzania wengi wamekuwa wakiifuata kwa ajili ya vipimo.

"Mradi huu umegharimia Sh. bilioni 18.2, fedha ambazo zimetolea na serikali, ni mradi wa kisasa na wa kimkakati kwa sababu ukitaka kuchunguza saratani kwa ufanisi zaidi, lazima utumie kifaa hicho ambacho kinapatikana hasa Ulaya, Marekani, Bara la Asia (India).

"Kwa Tanzania ilikuwa haiwezekani na ndio maana wagonjwa wengi walikuwa wanakwenda huko Ulaya au India kwa ajili ya kufuata kifaa hicho, kwa sasa kinachofanyika ni ufungaji wa mashine, hivyo kutumika rasmi itakuwa ni Machi mwaka huu.

"Tulikuwa na changamoto kubwa kwamba mtu anaweza kufika lakini wakati mwingine asigundulike mapema, lakini hii itagundua katika hatua za chembembembe, hiyo inamaanisha kwamba wagonjwa watakaopatikana itakuwa ni katika hatua za awali za ugonjwa mradi tu wawe na utaratibu wa wenyewe kuwahi.

"Lakini hata akitibiwa ili tujue kama saratani yake imeisha, ataingizwa tena kwenye kifaa hicho ili kujiridhisha.

Alisema kwa Tanzania kuleta kifaa hicho kutaokoa fedha ambazo wagonjwa wengi kutoka Tanzania wamekuwa wakizitumia kwenda kutibiwa nje ya nchi.

"Mbali na kwamba tutapunguza Watanzania kwenda kutibiwa nje ya nchi, pia tutaongeza idadi ya wananchi wanaotoka Kanda ya Afrika Mashariki na Kati, hata Kusini mwa Jangwa la Sahara kufika Tanzania kwa ajili ya kufuata kifaa hiki," alisema.

Mkurugenzi wa Magonjwa Yasiyo ya Kuambukiza wa Wizaya ya Afya, Dk. Omary Ubuguyu, alisema moja ya sababu zinazochangia kuongezeka kwa magonjwa hayo yasiyoambukiza ni kuwapo mazingira hatarishi, ikiwamo watu kutokufanya mazoezi.

Sababu nyingine aliitaja kuwa ni mtindo wa maisha hasa vyakula vinavyotumika ikiwamo chipsi, pia matumizi ya vileo kama pombe, sigara, shisha na vilevi vinginevyo.

## HABARI KITAIFA

# CRDB yakabidhi kituo cha mawasiliano Ocean Road

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya CRDB imekabidhi kituo cha mawasiliano kwenye Taasisi ya Saratani ya Ocean Road (ORCI) ikiwa ni matokeo ya fedha zilizokusanywa katika mbio za benki hiyo (CRDB Bank Marathon 2021).

Kituo hicho cha kisasa na cha kwanza kwa hospitali nchini, kilikabidhiwa mwishoni mwa wiki kwa uongozi wa taasisi hiyo mbele ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla aliyekuwa mgeni rasmi katika hafla hiyo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, alisema Benki ya CRDB ni mdau mkubwa wa maendeleo ya sekta ya afya nchini kupitia Sera ya Uwekezaji kwa Jamii ambayo inaelekeza benki kutenga asilimia moja ya faida yake kila mwaka kwa ajili ya kutatua changamoto katika sekta za afya, elimu, mazingira na uwezeshaji kwa wanawake na vijana.

Katika sekta ya afya, Benki ya CRDB imejikita zaidi katika kuboresha huduma za afya ya mama na mtoto na pia huduma za kibobezi, ikiwa ni pamoja na ufadhili wa ujenzi na uboreshaji wa vituo vya afya, wodi za wagonjwa na utoaji wa vifaa tiba kwenye vituo vya afya, zahanati na hospitali mbalimbali nchini.

"Mwaka 2020 Benki ya CRDB ilianzisha mbio za hisani zilizopewa jina la CRDB Bank Marathon kwa lengo la kusaidia jamii kwa kushirikisha wadau mbalimbali.

"Kupitia mbio hizi mnamo mwaka 2021, tukishirikiana na washirika wetu ambao baadhi tupo nao hapa, tulifanikiwa kukusanya takribani Sh. milioni 500 ambapo kati ya hizo, tulitenga Sh. milioni 102 kufadhili ujenzi wa Kituo cha Huduma kwa Wateja chini ya Taasisi ya Saratani ya Ocean Road ili kurahisisha ufikishwaji wa huduma, elimu na ushauri juu ya saratani kwa Watanzania wengi," alisema Nsekela.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Ocean Road, Dk. Julius Mwaiselage aliishukuru Benki ya CRDB kwa kusaidia ujenzi wa kituo hicho cha mawasiliano ambacho kinakwenda kuisaidia katika kutekekeleza malengo ya kuanzishwa kwake husuan upande wa kuongeza uelewa wa ugonjwa wa saratani, jambo ambalo ni muhimu katika mapambano dhidi ya ugonjwa huo.

Sehemu ya washiriki wa matembezi hayo ni mashujaa waliopona ugonjwa wa saratani ambao walisisitiza umuhimu wa kupima saratani mara kwa mara kwani kugundulika mapema kwa saratani kuna mchango mkubwa katika matibabu yake.

Akizungumza katika hafla hiyo, Makalla alisema serikali chini ya Rais Samia Suluhu Hassan imetenga fedha za kutosha kwenye sekta ya afya na kuhakikisha kunakuwa na mgawanyo mzuri wa vituo vya afya katika ngazi zote ili wananchi kutoka maeneo yote ya nchi wapate huduma bora za afya.

Makalla aliipongeza Benki ya CRDB na washirika wake kwa kufanikisha ujenzi wa kituo hicho kama walivyoahidi wakati wakihamasisha ushiriki wa mbio hizo.

# Mawaziri wawekwa kitimoto na CCM

**Na Mary Geofrey**

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, amehitimisha ziara yake ya siku tisa mkoani Morogoro kwa kuwataka mawaziri kujibu hoja za miradi ambayo utekelezaji wake umeonekana kusuasua na kuwa kero kwa wananchi.

Chongolo alihitimisha ziara hiyo jana sambamba na kuadhimisha miaka 46 ya kuzaliwa kwa CCM kwenye Uwanja wa Sabasaba mkoani Morogoro.

Sekta ambazo Chongolo alikutana na kero kwenye maeneo aliyopita ya vijiji, kata na wilaya za mkoa huo ni maji, umeme, barabara, afya, elimu, ardhi na kilimo.

Mawaziri waliotakiwa kujibu kero hizo ni Naibu Waziri Ofisi ya Rais - TAMISEMI, David Silinde, ambaye alijibu hoja ya mgawanyo wa walimu kwa usawa katika shule zote za serikali nchini.

Silinde alisema baada ya agizo la Chongolo, tayari wameshatoa barua 545 za uhamisho kwa walimu wa mkoa huo na kutenga Sh. milioni 607 kwa ajili ya kazi hiyo.

Kuhusu Shule ya Msingi Ngerengere ambayo ilikuwa haijakamilika, Silinde alisema wamepokea maelekezo na tayari wametenga Sh. milioni 100 kwa ajili ya kuikamilisha.

Kuhusu vifaa tiba kwenye zahanati na vituo vya afya mkoani hapa, Silinde alisema serikali imetenga Sh. bilioni 95.7 na tayari vifaa vimeshaagizwa kwa ajili ya kufungwa na kutoa huduma ya matibabu.

Kuhusu sekta ya maji, Chongolo alimtaka Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi, kujibu hoja ya tatizo la kukosekana maji kwenye baadhi ya maeneo ya mkoa huo, Naibu Waziri huyo akisema wizara inafanya kazi usiku na mchana ili wananchi wapate huduma hiyo.

Naibu wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ridhiwani Kikwete alisema kati ya mashamba 77 waliyokagua ambayo hayaendelezwi, 11 yamefutwa na hekta 2,025 zimegawiwa kwa wananchi.

Katika sekta ya mifugo, Chongolo alimtaka Naibu Waziri wa Mifugo, Abdullah Ulega kuwaeleza wananchi wa mkoa huo ni kwa namna gani wizara itamaliza migogoro ya wakulima na wafugaji ambao wanahamisha mifugo.

Ulega alisema wametenga hekta 500 kwa ajili ya wafugaji wilayani Mvomero na wamejenga majosho na kutengeneza mabwawa na kuchimba visima kwa ajili ya kutumiwa na mifugo ili kupunguza migogoro hiyo.

Waziri wa Kilimo, Hussen Bashe, akijibu hoja za wakulima kuwa na viwanda vya kuchakata mazao na kuwapo kwa soko la uhakika, alisema serikali inajenga viwanda vya kuchakata mazao ili kutoa ajira kwa vijana.

Kuhusu mfumuko wa bei, Bashe alisema tayari imewekwa mikakati miwili ambayo ni kutoa ruzuku ya mbolea kwa wakulima na kununua mazao ya wakulima ili kuyahifadhi ghalani na kuyauza kwa walaji.


CRDB BANK
*The bank that listens*

**REQUEST FOR EXPRESSIONS OF INTEREST (CONSULTING SERVICES)**

**FOR**
**WOMEN ENTREPRENEURS FINANCE INITIATIVE (We-fi) TRUST FUND – STRENGTHENING ACCESS TO FINANCE FOR WOMEN SMEs IN TANZANIA**

**Banking Industry/Financial Sector**

Financing Agreement reference: Women Entrepreneurs Finance Initiative (We-fi) Trust Fund

**Project ID No.**: G-TZ-H00-ZZZ-001

The CRDB Bank Plc has received financing from the African Development Bank toward the cost of the Women Entrepreneurs Finance Initiative (We-fi) Trust Fund – Strengthening Access to Finance for Women SMEs in Tanzania and intends to apply part of the agreed amount for this Grant No. G-TZ-H00-ZZZ-001 to payments under the contract for Strengthening Access to Finance for Women SMEs in Tanzania.

**The services included under this project are as mentioned below:-**

**Lot 1 – Enhance Customer Value Proposition (CVP) and include the below activities;-**

a. Diagnostic assessment (gender dis-aggregation of data)
b. Product enhancement (Financial & non-financial services)
c. Brand re-positioning (communication & brand recognition with WSME's)
d. Policy engagement & advocacy to enhance WSME's status.

**Lot 2 – MIS upgrade to improve on results based Monitoring and Evaluation and include the below activities;-**

a. An assessment of the current Result Based Measurement tools and the adequacy of the tools and systems to track lending and non-lending portfolio of activities.
b. To provide guidance on data clean and create sub segmentsof the Women's portfolio such as SME size, sector sub segment.
c. Jointly with relevant CRDB team, formulate outcomes and goals to improve on the reporting mechanism that includes gender target, including integrating the Bank's development outcome and reporting template
d. Recommend and upgrade the current MIS to improve results targets, monitoring for results, reporting findings, sustaining the M& E systems within CRDB Bank Plc.
e.

**Lot 3 – Non-Financial Services targeting WSMEs underpinned by a gender mapping exercise to identify the relevant value chains in which women are more participatory and will include the following:**

a. Education: Business and financial education in the form of interactive experiential learning programs for women entrepreneurship to improve and grow their businesses. Delivered either in person or digitally.
b. Business related information: This will include market research on key sectors and relevant updates on tax policy, regulation delivered to WSMEs through various channels e.g., frontline officers, web pages, publications.
c. Mentorship programs: Through direct interaction with knowledgeable resources such as business coaches, accountants, and legal experts, in person or digitally.
d. Networking and Markets: This will be delivered through in person networking events in close collaboration with women business associations, incubators and accelerators focused on the growth of WSMEs in Tanzania. The facilitation of digital networking tools that support WSMEs in connecting with peers and role models will also be leveraged, as well as recognition programs that showcase successful women entrepreneurs.
e. Business management technology: This will include financial management solutions such as cashflow management, payroll, invoicing, accounting, inter aiia.

The CRDB Bank Plc now invites eligible consultants to indicate their interest in providing these services. Interested consultants must provide information indicating that they are qualified to perform the services (brochures, description of similar assignments, experience in similar conditions, availability of appropriate skills among staff, etc.). Consultants may constitute joint-ventures to enhance their chances of qualification.

Eligibility criteria, establishment of the short-list and the selection procedure shall be in accordance with the African Development Bank's **Procurement Policy Framework dated October 2015,** which is available on the Bank's website at http://www.afdb.org. Borrowers are under no obligation to shortlist any consultant who expresses interest.

Interested consultants may obtain further information at the address below during office hours from 0800 hours to 1600 hours Monday through Friday, excluding public holidays .

Late Tenders, Tenders not received, and not opened and not read out in public at the Tender opening ceremony shall not be accepted for evaluation irrespective of the circumstances. Any application not received, not opened and not read out in public Tender opening ceremony shall not be considered for evaluation irrespective of the circumstances. All tenders shall be submitted only through the Email: **tenders@crdbbank.co.tz** , not later than **19th February 2022** at 1530 hours with Subject Title **"Women Entrepreneurs Finance Initiative (We-fi) Trust Fund – Strengthening Access to Finance for Women SMEs in Tanzania"**, late bid will be rejected.

All questions that may arise from the pre-qualification documents should be directed to CRDB Bank Customer service department.

**Email:** info@crdbbank.co.tz

**Copy to:** procurementdesk@crdbbank.co.tz

**Phone Numbers:** 0222197700; 0800008000; 0714197700; 0755197700; 0789197700.

**The Managing Director**
CRDB Bank Plc
CRDB Headquarters,
Plot No.25 & 26 Ally Hassan Mwinyi Road &
Plot No.21 Barrack Obama Road
**P.O. Box:** 268, 11101 Dar es Salaam, Tanzania
**Tel:** +255 (0) 22 211 7441 – 7
**Fax:** +255 (0) 22 211 6714
**Email:** info@crdbbank.co.tz
**Website:** http://www.crdbbank.co.tz

[1] If appropriate, In some cases, there may not be a project, but instead, only a specific consultancy services assignment.
[2] Recipient, in the case of grants
[3] For example, 0900 to 1700 hours

217264302

# Watumishi matatani ajali iliyoua 20

**Na Waandishi Wetu**

IDADI ya ndugu wa familia moja waliofariki dunia kutokana na ajali ya basi dogo la abiria na fuso iliyotokea wilayani Korogwe mwishoni mwa wiki imefikia 16 baada ya watoto wawili waliokuwa wanaendelea na matibabu kwenye Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Tanga (Bombo), kufariki dunia.

Kutokana na vifo hivyo, idadi ya waliofariki dunia katika ajali hiyo imefikia 20 huku ndugu wa familia moja wakitarajiwa kuzikwa leo Rombo mkoani Kilimanjaro.

Vifo vilivyoongezeka ni vya watoto wadogo wawili, Dorice Mrema na Tony Mrema ambao walikuwa wamelazwa kwenye Chumba cha Uangalizi Maalum (ICU) baada ya kuhamishiwa Bombo, wakitokea Hospitali ya Wilaya ya Korogwe (Magunga).

Jana Daktari wa Kitengo cha Dharura cha Hospitali hiyo ya Mkoa, Dk. Arafa Kachenje alisema watoto hao walifariki dunia kwa nyakati tofauti kati ya saa 10 jioni na saa nne juzi.

Ajali hiyo ilitokea usiku wa Februari 3, mwaka huu eneo la Magira Gereza, Wilaya ya Korogwe, Barabara ya Segera/Buiko na kusababisha vifo hivyo na majeruhi 12, ikihusisha lori la mizigo aina ya Mitsubishi Fusso, lenye namba za usajili T 673 CUC, lililogangana uso kwa uso na basi dogo aina ya Toyota Coaster, lenye namba T 863 DXN, lililokuwa limeubeba mwili wa marehemu Athanas Mrema (59) likiwa na waombolezaji 26.

Basi hilo lilikuwa linatoka jijini Dar es Salaam kwenda Kitongoji cha Kirungu-Mokala, Kata ya Kelamfua Mokala, Wilaya ya Rombo, ambako mwili wa Mrema ulitarajiwa kuzikwa.

Ndugu hao pamoja na majirani, walikuwa wanasindikiza mwili wa mwanafamilia huyo aliyefariki dunia Februari Mosi mwaka huu.

Kwa mujibu wa msemaji wa ukoo wa Mrema, Colman Mrema, miili ya ndugu wanne itazikwa sehemu moja na ndugu wengine ambao ni watoto wa baba wadogo na shangazi zao, watazikwa katika maeneo mengine tofauti wilayani humo.

"Kifo hiki kwa kweli kimetuhuzunisha maana ni msiba juu ya msiba na leo hii tulikuwa tumzike ndugu yetu Athanas. Ni msiba ambao haujawahi kutokea katika kijiji hiki na hata wilaya nzima, kwa kweli msiba ambao haulezeki kwa mtazamo wa kawaida," alisema.

### WATUMISHI MATATANI

Katika hatua nyingine, Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Mgumba, amewasimamisha kazi Mkuu wa Divisheni ya Afya, Ustawi wa Jamii la Lishe wa Halmashauri ya Korogwe, Salma Swedy na Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Wilaya ya Korogwe ya Magunga, Dk. Heri Kiwale kupisha uchunguzi, wakidaiwa kuchelewa kufika eneo la tukio, baada ya ajali hiyo kutokea.

Mgumba alitangaza uamuzi huo wa kuwasimamisha kazi maofisa hao jana baada ya kuzungumza na ndugu wa wafiwa waliokuwa kwenye Hospitali ya Magunga.

Kiongozi huyo alikerwa na kitendo cha ajali hiyo kutokea majira ya saa 4:30 usiku na watumishi wa hospitali hiyo kufika eneo la tukio saa 9:45 alfajiri.

### WAZIRI ATOA NENO

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yusuph Masauni, ambaye alikwenda jana kuwajulia hali majeruhi wa ajali hiyo, alisema dawa ya madereva wanaosababisha vifo na majeruhi kila uchao, itapatikana kutoka timu ya uchunguzi wa mfumo wa haki jinai iliyoundwa na Rais Samia Suluhu Hassan.

"Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ameunda tume ambayo pamoja na mambo mengine, itatushauri kufanya mabadiliko makubwa kwenye Jeshi la Polisi. Mabadiliko hayo ni pamoja na kuwa jeshi la kisasa litakalobaini na kuchukua hatua haraka dhidi ya ukiukwaji wa sheria za usalama barabarani.

"Tunaamini wakikamilisha hayo, madereva wanaokiuka sheria za usalama barabarani watakuwa na hofu na hivyo kuzingatia taratibu za usalama wanapokuwa barabarani na hivyo kupunguza ajali nchini," alisema Waziri Masauni.

***Imeandikwa na Godfrey Mushi (ROMBO) na Oscar Assenga (TANGA)***

# Adaiwa kuua dada wa kufikia, akamchoma kisu mama ubavuni

**Na Jenifer Gilla**

"ALIYEUA kwa upanga, atakufa kwa upanga!" Ni kauli ya Lonida Mosha, mkazi wa Mtaa wa Kimamba, Kata ya Makulumla, Halmashauri ya Ubungo mkoani Dar es Salaam, aliposimulia kifo cha mwanawe Erick Kwai (32) aliyeuawa na wananchi wa mtaa huo baada ya kudaiwa kumuua Anna Thomas (28) na kuutumbukiza chooni mwili wa binti huyo.

Akizungumzia tukio hilo, lililomuhusisha pia mama huyo kudaiwa kuchomwa kisu na mwanawe huyo, Lonida alisema amesikitishwa na kitendo alichokifanya mwanawe kwa kuwa alikuwa akiishi na Anna kama mtoto wake baada ya kumchukua akiwa ametelekezwa kilichokuwa Kituo cha Mabasi Ubungo miaka 17 iliyopita.

Alisema baada ya kumlea Anna kwa muda mrefu, alimwajiri kwenye biashara yake ya kuuza mtori.

Akisimulia tukio hilo, mama huyo alidai aliondoka nyumbani kwake juzi majira saa 11 alfajiri, akamuacha binti yake amelalala, na ilipofika saa nne asubuhi, alihisi kuna jambo halipo sawa kwa kuwa binti yake aliyekuwa hajafika ofisini, alimpigia simu bila mafanikio, ndipo alipoamua kurejea nyumbani kumwangalia.

"Nilipofika nikashangazwa kukuta majirani wamejaa nyumbani, nilipowahoji wakaniambia wanahisi Erick amemuua Anna kwa kuwa walisikia kelele za Anna kwa muda mrefu na nje kumetapakaa damu.

"Nilipomuuliza Erick 'Anna yuko wapi? Akanijibu ingia chumbani ukamwone Anna wako', huku akiwa ameshika kisu mkononi," alisimulia.

Alidai kuwa alisita kuingia ndani kwa kuhofia usalama wake kutokana na tabia na mienendo ya kijana wake na kwamba wakati anaendelea kumuuliza maswali, kijana huyo alimchoma kisu ubavuni na kupatwa na maumivu makali.

"Baada ya kunichoma kisu, alikimbilia ndani akafunga mlango, kitendo kile kiliwaudhi majirani, waliuvunja wakaingia ndani wakampiga hadi akafariki dunia.

"Kwa kweli mimi ninamlilia Anna, yule binti alikuwa na tabia nzuri sana, nimeishi naye kama mwanangu, kijana wangu alikuwa na matendo ya ajabu, sio kwangu tu hata kwa majirani," alidai Lonida.

Aliendelea kusimulia kuwa baada ya kijana wake kushambuliwa na majirani hadi kufa, aliingia ndani kumtafuta Anna bila mafanikio ndipo wakafuata alama za damu zilizokuwa zimemwagika kuanzia sebuleni hadi chooni walikouona mwili wake ukiwa umetumbukizwa ndani ya shimo la choo.

Mmoja wa mashuhuda wa tukio hilo, Dikson Mmari alidai kuwa majira ya saa nne asubihi, alisikia kelele kutoka kwa majirani kuwa Anna ameuawa na alipofika eneo la tukio alimkuta kijana huyo amefunga mlango, akivunja vyombo vilivyopo ndani huku akisema kuwa ameshamuua na hawawezi kumfanya kitu chochote.

Alidai kuwa kijana huyo alikuwa na matatizo ya akili kutokana na kuvuta bangi kwa muda mrefu, pia alikuwa akiogopwa na watu wa mtaa huo kutokana na tabia yake ya kufanya fujo na kuharibu mali za watu na kutishia kuwachoma visu.

Mwenyekiti wa mtaa huo, Ibrahim Mselem, alisema amesikitishwa na tukio hilo na kuwasihi wazazi waangalie mienendo ya watoto wao tangu wanapokuwa wadogo na kuikemea ili kuepukana na matukio hayo.

Alisema anamfahamu kijana huyo kama mgonjwa wa akili kwa kuwa alishampeleka hospitalini Machi mwaka jana ambako alipatiwa matibabu na kupewa dawa alizotumia kwa miezi mitatu tu kisha akaachana na dozi hiyo.

Akizungumzia tukio hilo, Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro alisema wamepata taarifa ya tukio hilo, lakini mtuhumiwa naye amefariki dunia kutokana na kipigo kutoka kwa wananchi.

"Mtu ambaye alipaswa kuwa mtuhumiwa, ameshapoteza maisha. Kwa kuwa watu walikuwa wanataka kumdhibiti na yeye alikuwa na kisu kwa hiyo wakachukua hatua za ziada ambazo zilipelekea kupoteza maisha," alisema.

Kamanda Muliro alitoa wito kwa jamii kwa kushirikiana na taasisi za dini, elimu na wasaikolojia kuzingatia malezi na maadili kwa watoto, ili kuepukana na matukio hayo.


WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI

**KUITWA KWENYE MAFUNZO KWA VITENDO (ATAMIZI)**

Tarehe 17 Disemba, 2022, Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Sekta ya Uvuvi) ilikaribisha maombi kutoka kwa vijana waliohitimu mafunzo ya uvuvi na ukuzaji viumbe maji ili waweze kujiunga na mafunzo kwa njia ya vitendo (Atamizi) kuhusu uvuvi na ukuzaji viumbe maji, na ujasiriamali. Mafunzo hayo yanatolewa kwa lengo la kuwawezesha vijana kujiajiri na kuongeza uzalishaji wa mazao ya uvuvi.

Orodha ya majina ya vijana waliochaguliwa kujiunga na mafunzo hayo yanapatikana kwenye tovuti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi; **www.mifugouvuvi.go.tz.**

Vijana waliochaguliwa wanatakiwa kuthibitisha ushiriki wao kabla ya tarehe **13 Februari, 2023, kupitia simu Na. 0716 098 893, 0767214229 na 0623915921.**

**Imetolewa na:**
**KATIBU MKUU - UVUVI**

# TANGAZO

EAST AFRICAN
CRUDE OIL
PIPELINE

## MAOMBI YA KUWASILISHA NIA KWA AJILI YA UTOAJI HUDUMA ZA UTHAMINI KATIKA MRADI WA BOMBA LA MAFUTA GHAFI LA AFRIKA MASHARIKI (EACOP) KUMB NA – REQ-00000094

Kampuni ya EACOP inazialika kampuni zenye uzoefu na sifa kuwasilisha maombi ya nia ya kutoa huduma za uthamini katika Mradi wa **Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).**

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litalofukiwa ardhini, linalokatisha mipaka ya nchi mbili ili kusafirisha mafuta ghafi kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda hadi Pwani ya Mashariki mwa Tanzania kwa ajili ya Kwenda katika Masoko ya Kimataifa. Bomba litaanzia eneo la Kabaale Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, hadi eneo la Chongoleani, Mkoani Tanga nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA MAWANDA YA HUDUMA:**

Utwaaji wa kudumu wa ardhi inayohitajika na Mradi wa EACOP unaelekea kukamilika. Wakati wa kipindi cha ujenzi, Wakandarasi wa Ujenzi watahitaji ardhi ya ziada ili kuitumia kwa muda kufanya kazi mbalimbali kando kando mwa mkuza wote wa Bomba la Mafuta. Hivyo, kampuni ya EACOP itahitaji kufanya makubaliano ya kutumika ardhi kwa muda ikihusisha vipande vya ardhi zaidi ya 250, vinavyokadiriwa kuwa na ukubwa wa kati ya ekari 0.5 hadi 1.25.

Kampuni ya EACOP inatafuta kampuni yenye uzoefu wa kutosha ili kuwezesha mchakato wa kupatikana ardhi ya muda itakayotumika kufanyia kazi kwa muda kando kando ya mkuza wa Bomba la Mafuta au kwa shughuli nyingine zozote za maandalizi ya Ujenzi.

**Mawanda ya huduma yatahusisha;**

- Kuthibitisha mahitaji ya ardhi ya muda na Timu za Ardhi na Uhandisi za EACOP katika kila eneo husika
- Kuzingatia matakwa ya ardhi ya muda kama yanavyoelezwa kwa kina katika Mpango wa Usimamizi wa Ardhi wa EACOP
- Kubainisha ardhi na wamiliki wake na kuwashirikisha kuhusu uhitaji wa kutumia ardhi hizo kwa muda
- Kufanya tathmini ya hali ya ardhi kabla na baada ya kutumia ardhi hiyo kwa muda.
- Kufanya makubaliano na wamiliki wa ardhi na watumiaji ili kutumika ardhi hizo kwa muda

**VIGEZO MUHIMU:**

Kampuni zinazowasilisha nia zinapaswa kutuma maombi pamoja na nyaraka zifuatazo::

- Uthibitisho wa Usajili kama Kampuni ya Uthamini toka Bodi ya Usajili wa Wathamini.
- Uthibitisho wa Usajili wa Wathamini wa Kampuni hiyo ya Uthamini toka Bodi ya Usajili wa Wathamini.
- Maelezo mafupi kuhusu uzoefu wa kutoa huduma za uthamini chini ya sheria za Tanzania na Viwango vya Fedha Kimataifa kwenye miradi mikubwa nchini Tanzania na maeneo ya vijijini
- Leseni ya biashara.
- Uthibitisho wa Usajili toka Mamlaka ya Mapato ya Tanzania (TRA) na Cheti cha Uthibitisho wa Malipo ya Kodi cha mwaka wa hivi karibuni.
- Usajili katika Kanzi Data ya Watoa Huduma wa Ndani ya EWURA (LSSP) au ushahidi thabiti wa maombi ya usajili wakati wa uwasilishaji wa maombi ya nia hii iliyotangazwa.
- Kufuata/kukubaliana na kanuni za Wazawa za Mambo ya Petroli za Tanzania.
- Wasifu wa watendaji watakaohusika katika Mradi ikiwa ni Pamoja na nakala za vyeti vyao, kiwango cha elimu, uzoefu na uwezo wa kutoa huduma inayohitajika.
- Uwezo wa kifedha wa kutoa huduma zinazohitajika ikiwa ni Pamoja na kuwakilisha hesabu za fedha za miaka mitatu iliyopita.
- Uthibitisho kutoka mfumo wa usimamizi wa QHSE, taasisi na mchakato kulingana na viwango vya ndani na vya ki-sekta vinayotumika kwa kazi hii.
- Uthibitisho wa kukubaliana na sera za kupinga rushwa, ufisadi ma Haki za Binadamu.

Kampuni zenye nia uwezo na rasilimali ya kutoa huduma zilizotajwa hapo juu zinatakiwa kutuma maombi ya nia yaliyoandaliwa kwa lugha ya Kiingereza pamoja na nyaraka zilizobainishwa hapo juu kupitia barua pepe: **procurement.tz@eacop.com (ukubwa usiozidi MB20) kabla au si zaidi ya saa 11:00 jioni Majira ya Afrika Mashariki, tarehe Jumatano 15 Februari 2023"** Kichwa cha cha barua pepe kiwe: [REQ-00000094] _ Kutoa huduma za uthamini katika Mradi wa EACOP.

Maombi yote ya kuonesha nia yawe kati ya kurasa 10 hadi 20.

Maombi yote lazima yawasilishwe kwa lugha ya Kiingereza.

**Muhimu**: EACOP itapitia na kuchambua nyaraka ziizotumwa na makampuni yalioonesha nia kulingana na EOI hii, na kisha kufanya tathmini kulighana na vigezo vya ndani vya EACOP ili kubaini makampuni yenye sifa yatakayojumuishwa kwenye orodha ya awali ya makampuni yenye vigezo. Mwaliko kwa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa Makampuni ya awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA). Kampuni ya EACOP LTD ina haki ya kuteua au kukataa kampuni na kubaki na maamuzi yake bila kutoa sababu kwa kampuni husika

---

IITA Transforming African Agriculture CGIAR

CENTRO INTERNACIONAL DE LA PAPA CIP

## POSITION ANNOUNCEMENT
## RESEARCH ASSOCIATE
## IITA-TZ2023-CIP-003-NRS-MWANZA

The International Institute of Tropical Agriculture (IITA) on behalf of the International Potato Center International (CIP) is seeking a Research Associate

**Background:** CIP is a not-for-profit international agricultural research organization with a global mandate to conduct research on genetic resources of potatoes, sweetpotatoes, and other Andean roots and tubers, crop genetic enhancement and improvement, integrated crop management and sustainable management of natural resources.

**Job Summary:** Agribusiness Research Associate to support business planning and marketing for sweetpotato seed at the Tanzania Agricultural Research Institute (TARI), Ukiriguru Center, and commercial seed producers. The Agribusiness Research Associate will implement activities aimed at expanding the market for quality seed to ensure that seed production is self-sustaining. This work is undertaken as part of the Sweetpotato Component of the Program for Seed System Innovations for Vegetatively Propagated Crops in Africa (PROSSIVA) implemented by the International Potato Center (CIP) and TARI. The Program for Seed System Innovation of Vegetatively propagated crops (VPCs) in Africa (PROSSIVA) will develop and validate packages of innovations to strengthen functional VPC seed systems and will work with partners to catalyze their scaling in five target countries of sub-Saharan Africa (SSA). The Sweetpotato Component aims to improve the crop's seed system through technological, marketing, and institutional innovations that deliver affordable quality seed of market-preferred varieties to actors in Tanzania in a timely manner. This will be implemented at the Lake Zone of Tanzania. The Agribusiness Research Associate will be based in Mwanza. This position will report to PROSSIVA's Principal Investigator for the Sweetpotato Component.

**Duty Station:** This is a Nationally Recruited Position, and the incumbent will be based in Mwanza, Tanzania.

**Core Responsibilities:**

- Work with key business oriented sweetpotato seed producers to develop strong value propositions for sweetpotato seed business.
- Train sweetpotato seed producers on entrepreneurship and business skills. This includes identifying potential markets to increase sales; and identifying market-preferred varieties and innovative marketing strategies.
- Guide the development and implementation of sweetpotato business plans for sweetpotato seed production at basic and quality declared seed (QDS) classes.
- Strengthen linkages within the sweetpotato seed value chain to facilitate business partnerships and attract investments.
- Provide technical backstopping to the sweetpotato seed producers' association.
- Validate TARI-led sustainable early generation seed (EGS) business models linked to the seed producer association.
- Develop journal articles and other communications materials.
- Any other deliverable related to developing sustainable business models for seed production assigned by the PI.

**Qualification, Experience and Key Skills**

- MSc in agri-business.
- Strong experience in establishing innovative public-private partnerships for increased sales in private seed industry.
- Experience with seed systems of roots, tubers and banana crops. Experience working on sweetpotato seed systems is an added advantage.
- Experience in leading a team in private industries to connect with farmers through contract farming.
- Knowledge on seed regulations and policies in Tanzania.
- Experience conducting effective competitive market research, quantitative and qualitative analysis; and implementation of best practices and processes.
- Experience in mapping value chain and analysis to identify potential business models and seed distribution channels.
- Sound knowledge of TARI and CIP's development and planning processes.
- A minimum of 5 years' experience working with large diverse teams.

**General information:**

The initial contract for the position is for two years: renewable subject to performance and availability of funds. The duty station for the position will be IITA in Dar es Salaam. This is a nationally recruited position and IITA offers a competitive remuneration package.

Applications: Applications including curriculum vitae, copies of certificates, telephone number, email address, and names and addresses of two referees should be sent to the Country Representative, IITA-Tanzania, Plot No. 25, Mwenge – Coca-Cola Road, Mikocheni Industrial Area P.O. Box 34441, Dar es Salaam, Tanzania or by email to **IITA-Tanzania@cgiar.org**

Applicants are requested to please indicate the reference number for the position as indicated on the heading of the announcement in your application as well as on the subject of your email if sending by email. If sending by post or hand delivery, please indicate the reference number on your application as well as on the left-hand side of your envelope. **Please note that any applications without the reference indicated will be automatically disqualified.**

**Closing date:** Two weeks from the date of advertisement appearing in the newspaper. Please note that only shortlisted candidates will be contacted.

217262202

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ligi Bara nafasi ya 5 ubora Afrika, waamuzi bado tatizo

**SHIRIKISHO** la Kimataifa la Historia na Takwimu za Mpira wa Miguu (IFFHS) limeitangaza Ligi Kuu Tanzania Bara kuwa ya tano kwa ubora barani Afrika na ya 39 duniani kwa mwaka 2022, ikipanda kutoka nafasi 10 Afrika na ya 62 duniani, nafasi iliyokuwapo mwaka mmoja kabla.

Tuna kila sababu ya kulipongeza Shirikisho la Soka nchini (TFF) na Bodi ya Ligi Tanzania (TPLB) kwa usimamizi mzuri na kutengeneza mazingira safi na rafiki kwenye ligi hiyo hadi kuisaidia kupaa na kuzifunika ligi kubwa kama za Afrika Kusini, Zambia, Angola na Tunisia.

Japo kwa wengi inakuwa vigumu kuamini ni kweli Ligi Kuu Tanzania Bara imestahili nafasi hiyo, lakini ni wazi vipo vigezo vingi vimezingatiwa na IFFHS kabla ya kuona Tanzania inastahili nafasi hiyo kwa sasa, hivyo tukubaliane na waliofanya utafiti na wenye kupinga wapinge kwa utafiti.

Katika hilo ni wazi kitendo tu cha Ligi Kuu Bara kuvutia wachezaji wengi wa kigeni kuja kucheza soka hapa nchini hususani Afrika Magharibi ambao kwa muda mrefu wamekuwa wakiamini maisha bora ya soka yapo Ulaya na Afrika Kaskazini maarufu nchi za Kiarabu, ni jambo la kuamini kwamba kweli ligi yetu inakua na inaendelea kupiga hatua.

Pia, awali ilikuwa wachezaji wakigeni wakija kucheza soka nchini, wengi watakuwa wa ukanda huu huu wa Afrika Mashariki na Kati na wakitua kuzichezea Simba ama Yanga tu, kitu ambacho kwa sasa ni tofauti kabisa kwani wametapakaa katika kila zote na ndio maana tunaona Wabrazil wenye viwango bora wakiitumikia klabu kama Singida Big Stars.

Lakini mafanikio ya Klabu ya Simba kutinga hatua ya robo fainali ya michuano ya kimataifa mara tatu, na kuiwezesha Tanzania kuingiza timu nne kwenye michuano ya Shirikisho barani Afrika (CAF), na msimu huu timu mbili zikitinga hatua ya makundi Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho, Simba na Yanga ni mambo ambayo yalizoeleka kwa nchi za Magharibi mwa Afrika na Kaskazini.

Hivyo, pamoja na mafanikio hayo yote na mengine, bado TFF na TPLB, zina kazi ya kufanya ili kuendana na kasi hiyo ya soka letu kukua, hususan kumulika zaidi changamoto ya waamuzi ambao wanaonekana kuwa gonjwa sugu katika ukuaji wa mpira wetu.

Hii ni kutokana na kushuhudia kila uchao waamuzi wengi wakifungiwa, na hawa ndiyo ambao mashabiki wengi wanadai kusababisha soka la Tanzania kudumaa na kupoteza mvuto na wao kupoteza matamanio ya hudhuria uwanjani lakini kuwa kikwazo kwa wawekezaji kuongezeka.


Ni wazi ni vigumu kwa wawekezaji kujitokeza kuweka fedha zao katika mchezo ambao mtu mmoja tu anaweza kuamua matokeo ya timu kushinda ama kupoteza kwa kufinyanga sheria 17 za soka duniani, hivyo sekta hiyo inahitaji maboresho makubwa zaidi ili soka la Tanzania kuweza kupiga hatua.

Tunaamini kama TFF na TPLB kwa kushirikiana na Chama cha Waamuzi nchini (FRAT), wakielekeza nguvu zao katika kuzalisha waamuzi wengi na bora huku wakiboresha maslahi yao, ligi yetu itawashangaza wengi kwa kwa kupiga hatua zaidi na kuwavutia wachezaji wakubwa na wawekezaji.

Suala la ubovu wa waamuzi hili halihitaji mjadala, lipo wazi na ndiyo maana ni nadra kuona waamuzi kutoka Tanzania wakichaguliwa kwenda kuchezesha michuano yoyote mikubwa ya CAF, kama ilivyo kwa wenzetu wa Afrika Mashariki na Kati, Kenya, Uganda, Burundi na Rwanda ambao wamekuwa wakipata nafasi hizo mara kwa mara tena kwa idadi kubwa.

Tunatamani kuona kikifika kipindi kwa waamuzi wenyewe kujitathmini na kurejea sheria na kanuni zinazowaongoza katika kazi yao ili kulinda heshima na kumulika maslahi makubwa zaidi wakilenga fursa ya kuchezesha mechi kubwa na si za CAF tu bali hata za Fifa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Waamuzi wanabadilika, makosa ya kibinadamu kwa wachezaji

Na Adam Fungamwango

**KABLA** sijaenda mbali napenda kutoa pongezi kubwa kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Waamuzi nchini, Nassor Hamdoun ambaye ni mwamuzi wa zamani wa kimataifa kwa kusimamia vema waamuzi wanaochezesha Ligi Kuu Tanzania Bara kiasi kwamba sasa hatusikii mashabiki na wadau wa soka waliwalalamika sana.

Msimu uliopita na mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu kulikuwa na malalamiko mengi kuhusu waamuzi kutokana na maamuzi yao ambayo yalionekana kuwa ya utata na ya kujirudia rudia, ambayo yalikuwa yakivikwa nguo ya 'makosa ya kibinadamu.'

Kilichoonekana ni kama waamuzi walikuwa wakishindana kufanya makosa. Huyu akikosea leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, mwingine atakosea kesho kwenye Uwanja wa CCM Kirumba. Kesho kutwa yupo mwingine atakosea Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa Lindi. Ilikuwa ni kama utamaduni, huku mashabiki, wapenzi, wadau wakiwamo waandishi wa habari na wachambuzi wakipiga kelele.

Kwa mara ya kwanza nilimsikia Hamdoun akikiri kuwapo tatizo na hata alipokuwa akiongea, alionyeshwa kukerwa na hilo.

Muda si mrefu yeye na kamati yake walianza kuchukua hatua kwa kuanza kuwafungia baadhi ya waamuzi wakiwamo wale maarufu kuchezesha Ligi Kuu na mechi kubwa, wakiwa pia na beji za Fifa.

Hamdoun alisema kabisa kuwa makosa yalikuwa mengi kiasi kwamba inafikirisha kama kweli ni ya kibinadamu, kwani wamekuwa na mafunzo ya mara kwa mara, lakini wanapokwenda kuchezesha wanarudia makosa yale yale.

Kwenye mechi za mwishoni mwa mzunguko wa kwanza na wa pili wameonekana waamuzi wengi wapya vijana, wakiwa na baadhi ya wakiwamo wa zamani wachache ambao hawakuwa na majina makubwa.

Cha kushangaza ni kwamba waamuzi hawa wameonekana kuchezesha mechi mbalimbali za Ligi Kuu kwa ubora wa hali ya juu kiasi kwamba, kwa siku za karibuni hatusikii makocha, wapenzi na mashabiki wakiwalalamika.

Timu zinacheza mmoja anafungwa, wachezaji, makocha na viongozi wanakubali kuwa walizidiwa. Husikii kuwa ni mbeleko, au makosa ya waamuzi. Kwenye mitandao ya kijamii hakuna zile video fupi za makosa ya waamuzi kama ilivyokuwa zamani na hata wachambuzi sasa kwenye vipindi wanachambua mpira na wachezaji, badala ya kipindi kizima kuongelea madudu ya waamuzi.

Hamdoun mwenyewe akikaririwa hivi karibuni akisema hayo ni mapinduzi makubwa na wataendelea kulisimamia hilo.

Alisema hayo yametokana na utayari wao na kuona soka la Tanzania linasonga mbele na wamekuwa wakipokea na kuyafanyi kazi maoni ya wadau wa soka, wakiwamo waandishi wa habari na wachambuzi.

Kiongozi huyo kama akiendelea kukaa hapo kwa muda mrefu na yeye mwenyewe akaendelea na dhamira hii, soka letu linaweza kupanda tena juu, baada ya kuwa wa tano, msimu ujao na mingine Shirikisho la Kimataifa la Historia na Takwimu za Mpira wa Miguu (IFFHS), linaweza kuipandisha Ligi Kuu ya Tanzania kutoka hapo ilipo na kwenda juu zaidi.

Hiki ndicho kilikuwa kilio kikubwa cha wapenzi wa soka, kwani walitaka maamuzi ya haki. Na kweli sasa yanaonekana kiasi kwamba kwa sasa kumekuwa na utani kuwa makosa ya kibinadamu yamehama kwa waamuzi na kutua kwa wachezaji.

Wana maana kuwa wachezaji wengi kwa sasa wamekuwa wakifanya makosa mengi yanayosababisha timu zao kufungwa. Makosa hayo ni kama yale ambayo waamuzi wengi waliofungiwa walikuwa wakiyafanya na baadhi ya timu hasa zile kubwa kunufaika.

Kwa wachezaji haina tatizo kwa sababu ni wao wenyewe, anafanya kosa timu yake inafungwa, baada ya hapo yeye atajuana na kocha wake. Na wakati mwingine ni lazima kosa lifanyike ili bao lipatikane.

Kilichokuwa kinawasikitisha wengi ni waliokuwa wanatakiwa kutoa maamuzi ya haki kuwa na makosa mengi ambayo yanafikirisha.

Unajiuliza hawa na sasa ambao wengi hawana hata uzoefu, ni kitu gani walichozidi kiasi cha kuchezesha vizuri?

Hata hivyo, natoa angalizo kwa Hamdoun na kamati yake kuendelea kuwakumbusha na kuwafuatilia kwa sababu waamuzi hawa pia nao ni binadamu, wanaweza baadaye wakajisahau na kuanza kufanya mambo yale yale. Lakini kwa hili Kamati ya Waamuzi wanastahili pongezi.

# ‘WanaCCM waliokosa nafasi za uongozi waache nongwa’

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MLEZI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Kaskazini Unguja, Dk. Tulia Ackson, amewataka waliogombea nafasi za uongozi na kushindwa, wasiwe na nongwa na kuendelea kutoa ushirikiano kwa chama hicho.

Alitoa rai hiyo jana wakati wa Kongamano la Miaka 46 ya CCM lililofanyika Mahonda kwenye ofisi za Mkoa wa Kaskazini Unguja za chama hicho.

Dk. Tulia ambaye ni Spika wa Bunge la Tanzania, alisema kuwa uchaguzi wa chama hicho umemalizika, hivyo ni vyema kushirikiana katika kukijenga.

Mlezi huyo aliwataka viongozi wote waliochaguliwa katika uchaguzi wa chama, kutowadharau wale ambao waligombea na kushindwa kwa kuwa uongozi ni kupokezana vijiti.

“Leo upo wewe kesho atakuwapo mwingine, sio kama nafasi uliyoipata utakaa nayo maisha, hivyo ni vyema kuonyesha ushirikiano kwa wanachama wote,” aliagiza Dk. Tulia.

Alisema kazi kubwa imefanywa na marais wote wawili wa Zanzibar na Tanzania katika kuiletea maendeleo nchi, hivyo wanachama wa mkoa huo wanapaswa kutokuwa wanyonge bali watembee kifua mbele kueleza mafanikio hayo.

Wakati akiwa katika ziara mkoani huko, Dk. Tulia alikabidhi boti saba za uvuvi pamoja na vifaa vyake kwa vikundi saba vya ushirika vya mkoa huo, akiwataka wanaushirika wa vikundi hivyo kuvitunza ili kudumu kwa muda mrefu na kuendelea kupata kipato cha kujikwamua kiuchumi na kuondakana na umaskini.

“Boti mlizokabidhiwa ni za kisasa na zina vifaa vya kisasa, hamna haja ya kuhangaika kutafuta samaki waliopo baharini maana vifaa mlivyopewa vinawaelekeza samaki walipo,” alisema.

Mjumbe wa Kamati ya Siasa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Ayoub Mohamed Mahmoud, alisema mkoa huo utaendelea kutekeleza ilani ya CCM kupitia viongozi waliochaguliwa.

Ayoub ambaye ni Mkuu wa Mkoa huo, alisema katika miaka 46, serikali ya CCM imejenga hospitali za mikoa na hakuna mwananchi anayetembea zaidi ya kilomita tano kufuata huduma za afya katika mkoa huo.

Alisema kuwa licha ya kuwapo changamoto kwa upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama, serikali inaendelea kuchukua jitihada mbalimbali ili huduma hiyo ipatikane kwa wakati.

Mwenyekiti wa CCM wa Mkoa huo wa Kaskazini Unguja, Iddi Khamis, alisema mkoa huo una utaratibu wa kutoa mafunzo kwa watendaji wa chama hicho ili kila mmoja atimize wajibu wake na chama hicho kupata ushindi wa kishindo katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (wa tatu kulia), akionyesha fungo ya moja ya magari yatakayotolewa kwa washindi wa promosheni ya ‘SimBanking’ ya benki hiyo, wakati wa uzinduzi wake uliofanyika mwishoni mwa wiki kwenye viwanja vya Zakhiem Mbagala, jijini Dar es Salaam. Katika promosheni hiyo, wateja wa Benki ya CRDB watakaofanya miamala yao kwa njia ya ‘SimBanking’ wataingia katika droo itakayowawezesha kushinda zawadi za magari, simu za mkononi pamoja na pesa taslimu kwa kipindi cha miezi kumi. Wengine pichani ni Ofisa Mkuu wa Biashara, Boma Raballa (kushoto), Mkurugenzi wa Mawasiliano, Tully Esther Mwambapa (wa tatu kushoto), Mkuu wa Kitengo cha Masoko, Joseline Kamuhanda (wa pili kulia), Meneja wa Kanda ya Mashariki, Badru Idd pamoja Meneja wa tawi la Mbagala, Nerea Igogo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Miili ya ajali na kesi za polisi yaigharimu Muhimbili

**Na Christina Mwakangale**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH), imesema kwamba kati ya changamoto inayokumbana nayo ni pamoja na kutoa misamaha, kugharamia huduma ya uchunguzi wa miili iliyotokana na ajali na ile ya kesi za polisi.

Imebainisha kuwa hadi sasa imekwishafanya uchunguzi wa aina hiyo (postmoterm) zaidi ya mara 400 na kila uchunguzi gharama yake ni Sh. 250,000 na kwamba misamaha pekee imefikia Sh. bilioni 9.8 kuanzia mwezi Julai hadi Desemba 2022, ikiwamo kuhudumia tiba kwa wafungwa.

Mkurugenzi Mtendaji wa MNH, Prof. Mohamed Janabi, alibainisha hayo mwishoni mwa wiki hospitalini huko alipowasilisha taarifa ya mafanikio na changamoto zilizojitokeza kwa mwaka wa fedha ulioanza Julai 2022.

Prof. Janabi akiwasilisha taarifa hiyo mbele ya Kamati ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, alisema kuwa pamoja na hospitali hiyo kuimarisha mifumo na kuziba mianya ya misamaha ili itumike kwa walengwa tu, ipo ambayo haipekuki.

“Bajeti inaweza kuongezwa na serikali ili kuhudumia gharama hizi, si lazima fedha zije kwetu moja kwa moja. Hivi sasa deni la MNH tunadaiwa Sh. bilioni 56.6 likitokana na Sh. bilioni 40 washitiri na stafu ni Sh. bilioni 16. Tumeshalipa deni Sh. bilioni 21.1 na tumeajiri wapya 38 wakiwamo waathiriwa wa methadone,” alisema.

Prof. Janabi alitaja changamoto nyingine ni idadi kubwa ya wagonjwa wasio na bima ya afya, wingi wa ndugu wanaokwenda kuona wagonjwa wanaofika 4,000 muda wa kuona wagonjwa, jambo linaloongeza msongamano MNH.

“Mfano, utafiti uliofanywa kubaini chanzo cha msongamano ikiwamo magari, ulibaini wapo wanaokuja kupaki humu ndani MNH, si wagonjwa wala ndugu, wanaacha gari wanatoka na kupanda mwendokasi kwenda mjini kufanya shughuli zao mjini. Kwa siku tuna magari 3,500,” alisema Prof. Janabi.

“Gharama kubwa za vitendanishi, vipimo, dawa kutokana na mfumuko wa bei ni changamoto. Mikataba ya MNH na washirika iko palepale ila gharama za utoaji huduma ziko juu na ikizingatiwa wagonjwa wanaohudumia zaidi ya asilimia 80 ni wa NHIF,” alisema Prof. Janabi.

Mjumbe wa Kamati hiyo na Mbunge wa Nanyamba (CCM), Abdallah Chikota alisema utaratibu uwekwe na Wizara ya Afya ili kuangalia namna ya kushughulikia utoaji huduma kwa msamaha kwa kuwa imekuwa ni changamoto kubwa kwenye taasisi nyingi.

“Misamaha imekuwa kati ya changamoto kwenye taasisi nyingi, kuwe na utaratibu wa namba ya kumpata mwenye vigezo vya kupatiwa msamaha kupunguzia deni hospitali,” alisema Chikota.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Stanslau Nyongo, aliipongeza MNH kwa kazi ambayo inayoendelea kuitoa kwa jamii, akisifu zaidi mafanikio katika usimamizi wa fedha na kujigharamia matumizi mengine tangu menejimenti mpya iingie madarakani.

## KABWELA



# Polisi yalisaka genge la waliopora milioni 100/-

**Na Mwandishi Wetu**

JESHI la Polisi Mkoa wa Kipolisi Ilala linamsaka Godfrey Chacha na genge lake kwa tuhuma za kuvunja baa ya Big Mountain na kuiba mali za zaidi ya Sh. milioni 100.

Akizungumza na waandishi habari ofisini kwake mwishoni mwa wiki, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kipolisi Ilala, Kamishna Msaidizi wa Polisi Debora Magiligimba (pichani), alisema jeshi hilo linamtafuta kwa nguvu zote mahali alipo mtuhumiwa huyo na wenzake.

“Hakuna mhalifu yeyote anayeweza kulikimbia Jeshi la Polisi na kama amekimbia, popote pale alipo ajisalimishe haraka kituo chochote cha polisi kwani hawezi kuwa salama, atatiwa nguvuni tu,” alisema Kamanda Magiligimba.

Alisema tayari taarifa imetolewa polisi na kupewa namba RB STK/RB/12887/2022 kwa madai ya kuvunja, kuharibu na kuiba mali.

Alisema taarifa za awali zinadai kuwa mtuhumiwa huyo alikimbilia Serengeti mkoani Mara, Kamanda Debora akisisitiza kuwa ni vyema akajisalimisha kabla hajatiwa nguvuni na mamlaka.

Kamanda huyo alidai Godfrey alishirikiana na Michael Chacha, Elizabeth Kiguha, Joseph Nyagare na Ester Kamando usiku wa kuamkia Desemba 28, 2022 kwa kuvunja baa hiyo. Watuhumiwa hao wanashikiliwa na polisi.





Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, akishuhudia jana utiaji saini wa mikataba sita ya ujenzi wa miradi ya maji kati ya RUWASA na makandarasi inayojengwa mwaka huu 2022/2023 itakayogharimu Sh. bilioni 7.562 ambayo ikikamilika itahudumia watu 77,767. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

## RC atatua mgogoro uliodumu miaka 30

**Na Thobias Mwanakatwe,**

SINGIDA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, amemaliza mgogoro kati ya wananchi wa eneo la Kititimo, Kata ya Mungumaji, Manispaa ya Singida na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) uliodumu kwa zaidi ya miaka 30 na kuagiza eneo hilo lipimwe upya na kila mmiliki apewe hati.

Serukamba (pichani) alitoa maagizo hayo juzi alipofuatana na viongozi wa Kamati ya Ulinzi na Usalama kwenye eneo hilo lenye ukubwa wa ekari 132.

“Maagizo yangu ni kwamba eneo lote hili lenye mgogoro lilikwenda kutumika na itatolewa hati kwa ajili ya shule, Kanisa la KKKT na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Manispaa ya Singida (SUWASA),” alisema.

Serukamba pia alisema wananchi waliojenga nyumba ndani ya eneo lenye mgogoro na kuishi kwa zaidi ya miaka 12, hawataondolewa.

Alisema kuwa kwenye eneo hilo litakalopewa na kuweka alama za mipaka (bicons), mwananchi atakayebainika kuzitoa, hatua kali zitachukuliwa dhidi yake.

Kaimu Ofisa Mipango Miji Manispaa ya Singida, Christian Kasambala, alisema kuwa kwa muda mrefu wameshindwa kupima eneo hilo kutokana na kutishiwa maisha na wananchi wanaodai eneo hilo ni mali yao huku ukweli ni kwamba linamilikiwa na KKKT tangu mwaka 1955.

# Bil. 4.8/- zakamilisha mradi wa maji Mshikamano

**Na Joseph Mwendapole**

MRADI wa maji wa Kata ya Mshikamano jijini Dar es Salaam uliogharimu Sh. bilioni 4.8, umekamilika kwa asilimia 99, ukitajwa kuchangia kwa kiwango kikubwa kupunguza shida ya maji.

Mradi huo una uwezo wa kusafirisha lita milioni 23,300 kwa siku ambazo zitatosheleza mahitaji ya wananchi 180,000 wa maeneo ya Kata ya Mshikamano, Mpiji - Majohe, Msakuzi Kusini, Msakuzi A, Machimbo, Majengo Mapya kwa kipindi cha miaka 20 ijayo.

Mwishoni mwa wiki, Mhandisi wa Miradi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), Ishamel Kakwezi, alibainisha hayo alipozungumzia mradi huo.

Kakwezi alisema utekelezaji wa mradi huo umegharimu Sh. bilioni 4.8. Kati yake, Sh. bilioni 2.5 ni fedha kutoka Serikali Kuu kupitia mfuko wa kukabiliana na athari UVIKO-19.

Alisema katika kuhakikisha lengo la kuboresha huduma linatimia, serikali ilibuni na kutekeleza mradi mkubwa wa kusambaza maji kwa wakazi wa Wilaya ya Ubungo, kata za Mbezi, Kibamba na Mshikamano ambazo zilikuwa na uhitaji mkubwa wa huduma ya majisafi.

Alisema kutokana na kuwapo uhitaji huo, DAWASA ilianza kazi ya kusanifu mradi wa maji wa Mshikamano kwa lengo la kukidhi mahitaji ya maji kwa wananchi wa maeneo tajwa ambao hawakuwa na huduma hiyo.

Alisema mradi wa Mshikamano unatarajiwa kuwa suluhu kubwa ya ukosefu wa maji kwa wananchi wengi ambao hawana huduma ya maji.

“Baada ya usanifu wa mradi, serikali kupitia Wizara ya Maji ilitia saini mkataba wa utekelezaji wa mradi na mkandarasi wa Kampuni ya M/S Advent Co. Ltd mwezi Oktoba mwaka 2021 ili kuashiria kuanza kwa utekelezaji rasmi wa mradi.

“Baada ya utiaji saini, kazi ya utekelezaji wa mradi ilianza rasmi mwaka 2021 kwa kufanya maandalizi ya awali ya vifaa vya utekelezaji wa mradi (mobilization) pamoja na vifaa, mitambo ya utekelezaji, wafanyakazi pamoja na uandaaji wa mpango kazi inayoendana na matakwa ya mkataba,” alisema.

Aliongeza kuwa mradi huo ni miongoni mwa miradi ya kimkakati iliyopangwa kutekelezwa na DAWASA kwa mwaka 2021/2022 ili kukidhi agizo la serikali la kuhakikisha ifikapo mwaka 2025 upatikanaji wa huduma ya maji unafikia asilimia 85 kwa maeneo ya vijijini na asilimia 95 kwa maeneo ya mijini.

Kakwezi alisema utekelezaji wa mradi umehusisha ulazaji wa bomba la chuma la inchi 16 kwa umbali wa kilomita 0.35 kutoka kwenye bomba la chuma la inchi 30 linalosafirisha maji kutoka kwenye Mtambo wa Ruvu Juu hadi kwenye kituo cha kusukuma maji eneo la Mbezi Inn.

“Pia mradi umehusisha ujenzi wa kituo cha kupokea na kusafirisha maji ambacho ndani yake kuna tangi la kuhifadhi maji lenye lita za ujazo 540,000 pamoja na ufungaji wa pampu, sambamba na ujenzi wa ofisi ndogo kwa ajili ya waangalizi wa kituo,” alisema.

Kiongozi huyo alisema kuwa kabla ya utekelezaji wa mradi, hatua mbalimbali za maandalizi zilitekelezwa ikiwamo kupima na kufanya utafiti wa ubora wa udongo (Geotechnical Investigation) kwenye eneo litakalojengwa tangi la maji pamoja na kituo cha kusukuma maji (pump house).

Alitaja hatua nyingine kuwa ni kuhakiki njia ya bomba (Pipe route survey) ili kuhakikisha umbali na uwezekano wa kupitisha bomba, pia kufanya mapitio ya usanifu wa miundombinu ya matangi na kituo cha kusukuma maji.

Alisema shughuli mbalimbali zilizofanyika kwenye eneo la mradi ni pamoja na ujezi wa bomba la chuma la inchi 16, pamoja na miundombinu yake kutoka kwenye bomba kuu la inchi 30 hadi kituo cha kusukuma maji (Booster Station),ujenzi wa kituo cha kusukuma maji (Booster pumping station), ujenzi wa tangi la ujazo wa lita milioni sita eneo la Mshikamano Juu.



## RUWASA yatia saini mikataba 15 ujenzi miundombinu ya maji

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

WAKAZI 24,129 wa vijiji 14 vya Mkoa wa Manyara, wanatarajia kunufaika na huduma ya majisafi, baada ya Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA), kutia saini mikataba 15 na makandarasi wa kujenga miundombinu ya maji.

Mkuu wa Mkoa huo Makongoro Nyerere, alisema katika utekelezaji wa miradi hiyo, vijiji 14 ndiyo vitaanza kuguswa ili kupunguza adha hiyo ya maji.

Makongoro aliyasema hayo wakati akizungumza na wakuu wa wilaya, wafanyakazi wa RUWASA na makandarasi waliopewa zabuni za kujenga miradi ya maji na wengine kusambaza vifaa vya ujenzi.

"Mkoa wetu kwa mwaka wa fedha 2022/2023, umeidhinishiwa shilingi bilioni 15.406 kutoka vyanzo mbalimbali, ambazo zitatumika kukamilisha miradi 28 inayoendelea, kujenga miradi saba mipya, kuongeza mtandao miradi nane, kuchimba visima 26 na kufanya usanifu wa miradi 53.

"Miradi hiyo itasogeza huduma ya maji kwenye vijiji vipya 40 kwa hiyo ifikapo Desemba mwaka huu idadi ya vijiji ambavyo havina huduma ya uhakika itapungua kutoka vijiji 91 hadi vijiji 51.

"Wazabuni ambao mmepewa kazi ya kusambaza vifaa vya ujenzi wa miradi hakikisheni mnasambaza vifaa vyenye ubora na vifaa vitapimwa ubora wake hivyo vifaa viwe vizuri visiwe na doa," alisema Makongoro.

Awali, Meneja wa RUWASA mkoani Manyara, Wolta Kirita, wakati akisoma taarifa ya utekelezaji wa shughuli za RUWASA, kuanzia Julai mosi mwaka jana hadi Januari 31, mwaka huu, alisema RUWASA makao makuu, ndio inaratibu ununuzi wa mabomba yote kutoka viwandani na uratibu huo uko katika hatua za mwisho.

Alisema kwa mkoa huo miradi inayonunuliwa mabomba ni Mdunga-Utwari, Einoth-Losinyai, Kiperesa, Esunguta, Aicho, Titiwi, Naberera-Losokonoi-Lorbeno, Orkesumet-Lerumo, Komolo-Olembele na miradi mbalimbali kwa mwaka huu wa fedha inaratibiwa na RUWASA makao makuu.

Alisema ununuzi wa vifaa vya ujenzi na makandarasi wa kujenga miundombinu ya maji unaratibiwa na bodi ya manunuzi ya kanda.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Genuine Limited, ambaye amepewa kandarasi hiyo, Loserian Mollel, alisema wana uwezo, kwamba hawatakuwa wababaishaji bali watafanya kazi kwa muda uliopangwa na kwa viwango.

# DC aagiza kuadhibiwa wanaolima vyanzo vya maji

**Na Allan Isack,** KARATU

MKUU wa Wilaya ya Karatu mkoani Arusha, Dadi Kolimba, ameagiza uongozi wa Bonde la Maji la Kati, kuwachukulia hatua za kisheria watu wanaofanya shughuli za kilimo katika vyanzo vya maji kwa kuwa wanafanya uharibifu wa mazingira.

Alitoa agizo hilo jana wakati wa upandaji miti katika kingo za Mto Baray kwenye eneo la Bonde la Ziwa Eyasi.

"Wale wote wanaotaka kulima kandokando ya Mto Eyasi na kukata miti naagiza ofisa mazingira na viongozi wa bonde kuwachukulia hatua kwa mujibu wa sheria za nchi yetu," alisema.

Alisema wamefikia hatua ya kupanda miti 1,000 pembezoni mwa bonde hilo kwa lengo la kulinda na kuhifadhi chanzo hicho cha maji.

"Hatua ya upandaji wa miti katika bonde hili imetokana na namna uharibifu wa mazingira ulivyofanyika hivyo natumia mamlaka yangu kuuagiza uongozi wa bonde kuchukua hatua za kisheria kwa wote watakaobainika kuharibu mazingira ikiwamo kulima pembezoni mwa vyanzo vya maji," alisema Kolimba.

**Wale wote wanaotaka kulima kando-kando ya Mto Eyasi na kukata miti naagiza ofisa mazingira na viongozi wa bonde kuwachukulia hatua kwa mujibu wa sheria za nchi yetu.**

Hata hivyo alisema wametekeleza jukumu hilo ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan akisisitiza suala la kuhifadhi na kutunza mazingira na Makamu wa Rais Dk. Philip Mpango akisisitiza wilaya zote kupanda miti milioni 1.5 mwaka.

"Tumepanda miti ili kuzuia uharibifu wa mazingira katika bonde hili la Mto Eyasi na jukumu la kuitunza tumelitoa kwa jumuiya ya watumiaji maji hivyo tunahakika itaendelea kutunzwa na itakuwa kwa ajili ya kuhifadhi chanzo hiki.

Mkurugenzi wa Bodi ya Maji Bonde la Kati, Danford Samson, alisema ili chanzo hiko kiendelee kuimarika waliadhimia kupanda miti ndani ya mita 60 kutoka kwenye kingo za chanzo kwa lengo la kuhifadhi, kukilinda na kuendeleza rasilimali za maji.

"Bodi ya Bonde tumejipanga kupanda miti katika vyanzo vya maji vikuu, vya kati, mito na pembezoni mwa ziwa kuhakikisha tunanusuru rasilimali adhimu ya maji iendelee kuwapo na itumike kwa matumizi mengine," alisema.

Alisema wamekuwa wakitoa elimu kwa wananchi na jumuiya za watumia maji juu ya kuhifadhi, kulinda na kusimamia rasilimali za maji hasa kwenye maeneo yao.

Aidha, alisema sheria inawaelekeza kuwa mtu yeyote anapovamia vyanzo vya maji achukuliwe hatua hivyo watafuata sheria kwa watakaobainika kufanya uharibifu wa miundombinu na kuvamia vyanzo.



Mkurugenzi Mtendaji wa Vodacom Tanzania Plc, Philip Besiimire (wa pili kushoto), akipokea maelezo kwa Mkurugenzi wa Jiji la Arusha, Hargeney Chitukuro (wa tatu kushoto), alipotembelea kituo cha afya cha Muriet jijini Arusha ili kujionea mafanikio baada ya kampuni hiyo kutoa msaada wa vifaa tiba vya kuhudumia watoto njiti mwaka 2020. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Shirika latoa mil.79/- ununuzi vifaa tiba, dawa, vitendanishi

**Na Jaliwason Jasson,** HANANG'

SHIRIKA la PharmAccess International, limeupiga jeki Mkoa wa Manyara katika ununuzi wa vifaa tiba, dawa na vitendanishi vyenye thamani ya Sh. milioni 79.712 kwa ajili ya kuboresha huduma za afya ya wajawazito na watoto.

Meneja Mradi wa Momcare unaotekelezwa na shirika hilo, Dk. Jonhson Mali, alisema vifaa tiba peke yake vilivyotolewa, vina thamani ya Sh.milioni 50.

Katika vifaa tiba hivyo, zimo mizani ya kupima uzito watoto wachanga na watu wazima, vifaa vinavyotumika kuzalisha wajawazito na kuwasaidia kuzuia maambukizi kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mwingine, vifaa vya kupima wingi wa damu na vifaa vya kupumzisha wagonjwa.

"Dawa na vitendanishi vilikuwa na zaidi ya shilingi milioni 29, ambavyo ni vifaa vya kupima malaria, vifaa vya kupima sukari na dawa za kuongeza wingi wa damu.

"Kimsingi, mradi wa momcare, ulikuwa wa miaka mitatu na uliisha mwaka jana, ila tumeona tufanye mwendelezo wa kutoa huduma na ndiyo maana tumeamua kutoa vifaa hivi ili viende vikasaidie vituo 33 vya Wilaya ya Hanan'g, ambayo ina uhitaji mkubwa.

"Lengo ni kuleta huduma bora ya mama na mtoto Hanan'g , kama vile mfumo wa taarifa wa dashboard utakaorahisishwa kupitia vishikwambi vilivyotolewa ambapo taarifa zitajazwa na zitafika kwa usahihi kwa wahusika," alisema Dk. Mali.

Akipokea msaada huo, kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Makongoro Nyerere, Katibu Tawala Msaidizi anayeshughulikia sekta ya afya, Dk.Damas Kayera, alisema vifaa hivyo vitasaidia kukusanya taarifa na kuboresha sekta ya afya.

Kwa mujibu wa Sera ya Afya ya Mwaka 2007, serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali na wananchi itaboresha miundombinu ili kuwawezesha wanawake wajawazito na watoto wachanga kufikiwa na kutumia huduma za afya.



# Wabunge CCM wapinga sababu mfumuko wa bei

**Na Vitus Audax**

WABUNGE wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wamepinga sababu zinazotolewa na serikali juu ya mfumuko wa bei za vyakula.

Hivyo wamewataka wakuu wa wilaya kudhibiti hali hiyo, huku wakikemea vitendo vya halmashauri kuwapanga machinga mbali na miji.

Mbunge wa Geita Vijijini, Joseph Kasheku 'Msukuma', akizungumza katika sherehe za kuzaliwa kwa chama hicho mkoani Mwanza juzi, alisema suala la mfumuko wa bei halitakiwi kuhusishwa na majanga ya vita na ugonjwa wa corona na kulitaka baraza la mawaziri kulijadili na kulimaliza tatizo hilo.

Alisema anachukizwa na majibu ya Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, juu ya mfumuko huo ambapo mchele uliokuwa ukinunuliwa kwa Sh. 1,200 mkoani Mwanza sasa unanunuliwa kwa Sh.3,500.

**Shule ya Msingi Sahara inaweza kuhamishwa pale patengenezwe sehemu maalumu kwa ajili ya machinga kufanya biashara.**

Alisema suala la machinga kurudi mitaani bado kuna uhitaji wa serikali kupitia halmashauri zao kubuni mbinu mbadala zitakazo wawezesha kufanya kazi katika maeneo ya mijini bila ya kuvuruga utaratibu.

"Shule ya Msingi Sahara inaweza kuhamishwa pale patengenezwe sehemu maalumu kwa ajili ya machinga kufanya biashara, vilevile kuna majengo ya Shirika la Nyumba hapa mjini wanakaa Wahindi na yamechakaa bomoeni maeneo machache wekeni machinga, machinga hawawezi kutoka nje ya mji tutazalisha vibaka," alisisitiza.

Kuhusu kupanda kwa gharama za maisha, Mbunge wa Kawe, Dk. Josephat Gwajima alisema serikali haiwezi kukwepa lawama za kupanda kwa bei za vyakula na kusema kuwa ili kufumbua tatizo hilo kuna haja ya serikali kupitia Wizara ya Kilimo kuweka usawa katika bei hizo ili kila mtu aweze kupata unafuu.

Aidha, aliwataka wananchi kutumia fursa hiyo kuwekeza katika kilimo cha umwagiliaji kutokana na uwapo wa Ziwa Victoria lenye maji ya uhakika wakati wote.

Mkuu wa Wilaya ya Ilemela, Hasani Masala, akizungumza katika mkutano alisema serikali inaendelea kufanya utaratibu wa kuwapatia maeneo rafiki wafanyabiashara ikiwa ni pamoja na kuwaandalia maeneo mahususi katika masoko makubwa yanayojengwa mkoani humo.



Baadhi ya wahudumu wa afya kutoka Idara ya Saratani katika Hospitali ya Rufani Kanda Bugando wakiendelea kutoa huduma ya vipimo mbalimbali vya magonjwa ya saratani ikiwamo saratani ya shingo ya kizazi, matiti na saratani ya tezi dume vilivyotolewa juzi katika hospitali hiyo bila malipo kufuatia maadhimisho ya Siku ya Saratani Duniani. **PICHA: VITUS AUDAX**

## Wafugaji walalamikiwa kuingiza mifugo shuleni

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MWALIMU Mkuu wa Shule ya Msingi Ndembezi iliyoko Manispaa ya Shinyanga, Mohamed Makana, amelalamikia wafugaji kuingiza mifugo kwenye maeneo ya shule hiyo na kusababisha uharibifu ikiwamo kula miti.

Alibainisha hayo juzi wakati Chama cha Tanzania Girl Guide Association, kilipokuwa kikiendesha kampeni ya upandaji miti 1,000 katika shule hiyo. Alisema shule hiyo haina uzio na kila wanapokuwa wakipanda miti imekuwa ikiliwa na mifugo na kusababisha kuendelea kukabiliwa na upungufu wa miti.

"Shule yetu hii ya Ndembezi kila tunapopanda miti imekuwa ikiliwa na mifugo, awali tulipanda miti 500 lakini yote iliiliwa, tunaomba viongozi wa serikali wadhibiti suala la wafugaji kuchungia mifugo maeneo ya shule, hasa nyakati za jioni sisi tukiwa hatupo wala wanafunzi,"alisema Makana.

Katibu Tawala Msaidizi, Sekta ya Uchumi na Uzalishaji Mkoa wa Shinyanga, Beda Chamatata, alionya tabia ya wafugaji kuchungia mifugo maeneo ya shule na kuwaagiza viongozi wa serikali za mitaa kuwakamata na kuwachukulia hatua ikiwamo kupanda miti yote ambayo imeliwa na mifugo yao.

Pia aliwataka wanafunzi na walimu waitunze miti yote ambayo imepandwa shuleni hapo, ili ipate kukua na kuondoa hali ya jangwa na kuilinda dhidi ya majanga mbalimbali pamoja na kupata faida ya kivuli.

Wakala mtetezi wa mradi wa msichana na mabadiliko ya tabia nchi kutoka Tanzania Girl Guide Association, Joyce Maganga, alisema wamekuwa wakiendesha kampeni ya upandaji miti shuleni na kwenye taasisi nyingine za serikali, ili kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi na athari za mazingira.

Alisema mbali na kupata miti 1,000 katika Shule ya Msingi Ndembezi, pia wameshapanda miti 300 katika Shule ya Msingi Ujamaa, miti 200 Shule ya Msingi Jomu.

Alisema kampeni hiyo ni endelevu ili kuendelea kuunga mkono juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan dhidi ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi, athari za mazingira na hewa ya ukaa.

## Wazazi wataja sababu kushindwa kuwapeleka watoto shule

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

BAADHI ya wazazi wa Kijiji cha Mseki Kata ya Bulungwa Halmashauri ya Ushetu mkoani Shinyanga, wamedai kushindwa kuwapeleka watoto wao shuleni waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza baada ya kukosa Sh.10,000 ya kulipia vipimo vya afya.

Walitoa malalamiko yao jana katika mkutano wa hadhara uliofanyika kijijini hapo ulioitishwa na Mbunge wa Ushetu, Emmanuel Cherehani, wakati akisikiliza na kutatua kero mbalimbali zinazowakabili wananchi.

Mkutano huo ulihudhuriwa pia na Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel.

Mmoja wa wananchi hao, Paschal Shimba alisema utaratibu uliowekwa wa kuwapima afya wanafunzi kabla ya kuanza masomo kwa gharama ya Sh.10,000 kwa kulipa katika vituo cha afya na hospitali ndiyo unasababisha wanafunzi waliochaguliwa kuanza masomo mwaka huu kuchelewa kuripoti.

"Hivi karibuni tumetangaziwa kuchukuliwa hatua za kisheria tutakaposhindwa kuwapeleka watoto wetu kuanza shule kwa wakati, tunahangaika kutafuta sare na vifaa vya shule lakini tutapofika hospitali katika vipimo vya mwanafunzi tunaombwa Sh.10,000 ambayo hatuna na tunarudi majumbani na watoto wetu,"alisisitiza.

Naye Rechal William alisema, kiasi hicho kimekuwa kikwazo kwao kukitoa hospitalini kwa ajili ya vipimo na badala yake ni vema wakakitoa katika maandalizi ya kununua vifaa vya shule.

Mbunge wa Ushetu, Emmanuel Cherehani alisema, ameshatoa Sh.milioni nane kwa ajili ya ujenzi wa matundu ya vyoo katika Shule ya Sekondari Bulungwa, fedha ambazo ni kutoka katika mfuko wa jimbo ili kuondoa msongamano wa wanafunzi katika vyoo wakati wa mapumziko.

Katibu Tawala, Timoth Ndanya, alisema serikali imetoa mwezi mmoja kwa wanafunzi waliochaguliwa kuanza kidato cha kwanza kwenda shuleni na nguo za nyumbani au alizozitumia shule ya msingi lengo asichelewe kuanza masomo.

Alisema suala la wazazi kuchangia Sh.10,000 katika vituo vya afya kwa ajili ya vipimo kwa wanafunzi ni utaratibu na itasaidia walimu kujua hali ya afya hususani kwa wanafunzi wa kike kutambua kama ni mjamzito au la.

**Walitoa malalamiko yao jana katika mkutano wa hadhara uliofanyika kijijini hapo ulioitishwa na Mbunge wa Ushetu, Emmanuel Cherehani, wakati akisikiliza na kutatua kero mbalimbali zinazowakabili wananchi.**

NIPASHE JUMATATU FEBRUARI 6 2023

Nipashe
Spotika



WACHEZAJI 10 BORA WALIOFUNGA MABAO MENGI TANGU 2020 12 - 13



# MECHI SITA MUHIMU ZA ARSENAL KUSHINDA TAJI EPL AU KUPOTEA

**LONDON, England**

MATUMAINI yenye mgawanyiko yalikuwa mengi kwa timu kutoka Kaskazini mwa Jiji la London kuelekea msimu wa 2022/23, lakini mashabiki wachache sana, walikuwa na imani ya Arsenal kurejea kwenye 'utukufu' wao chini ya kocha Mikel Arteta.

Arsenal kwa sasa wako katika nafasi nzuri kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu England, pointi tano mbele ya mabingwa watetezi, Manchester City kabla kikosi hicho cha Pep Guardiola kuvaana na Tottenham jana, hata hivyo, mechi hiyo itaifanya City kuwa mchezo mmoja mbele.

Kiwango chao hakijayumba licha ya kukosekana kwa mshambuliaji wao mkuu Gabriel Jesus, ambaye alibadilisha mashambulizi ya 'Washikabunduki' kabla ya Kombe la Dunia na Eddie Nketiah anacheza vizuri nafasi yake kwa sasa.

Ingawa wengine bado wanatabiri kifo chao, wengi wamegundua uhalali wa Arsenal kama mshindi wa taji la Ligi Kuu England msimu huu.

Lakini bado kuna safari ndefu katika msimu wa 2022/23 na hapa kuna mechi sita ambazo zitaamua Arsenal kutwaa taji la Ligi Kuu England msimu huu au kupoteza.

**#1. ARSENAL VS MAN CITY (15/02/23)**

Washikabunduki hao wamefuzu kila mtihani ambao wamekumbana nao msimu huu, lakini bila shaka huu utakuwa mgumu kwao. Wawili wa sasa bora zaidi watakutana kwenye Uwanja wa Emirates katika kile kinachotarajiwa kuwa usiku wa Jumatano wa kuamkia katikati mwa Februari.

Ni mechi ya kishindo huku Manchester City wakija mjini katika shindano litakalobainishwa kuwa la mapema katika mbio za ubingwa.

Arsenal ambao Jumamosi walipoteza kwa bao 1-0 ugenini dhidi ya Everton, watakuwa na matumaini kwamba uongozi wao bado uko sawa wakati itakapocheza mechi hizi...

**#2. LIVERPOOL VS ARSENAL (08/04/23)**

Umekuwa msimu mbaya kwa Liverpool hadi sasa. Kumekuwa na sababu nyingi katika kifo chao cha msimu huu 2022/23, na majeraha yana jukumu kubwa.

Wachezaji kama Luis Diaz, Diogo Jota na sasa Virgil van Dijk wamekuwa nje ya dimba kwa vipindi virefu, lakini kila mmoja wa wachezaji hawa anatarajiwa kurejea uwanjani katika kipindi cha pili cha msimu huu. Kwa hiyo 'Wekundu' hao wanaweza kuimarika kadri msimu unavyosonga na safari hii ya kuelekea Anfield haitakuwa rahisi sana kwa vinara hawa.

Uwanja wa nyumbani wa Liverpool haujawa ngome yao miaka mingi iliyopita, Arsenal haijapata ushindi ugenini dhidi ya Wekundu hao tangu mwaka 2012.

**#3. MAN CITY VS ARSENAL (26/04/23)**

Ingawa mechi ya kwanza ya Ligi Kuu kati ya pande hizo mbili huenda isiwe ya kuamua taji kama hilo, mchezo wa Aprili unaweza kuwa sawa ikiwa kila mmoja ataendelea na njia yake ya sasa.

Guardiola ametawala mchezo huo akiwa na mwanafunzi wake Arteta tangu achukue mikoba ya Washikabunduki hao, lakini Mhispania huyo atakuwa na wakati mgumu kupata matokeo dhidi ya timu bora pale Etihad.

Manchester City haijafungwa na Arsenal kwenye Ligi Kuu tangu mwaka 2015, huku wakishinda mara 12 katika mechi 13 zilizopita kwenye mashindano yote.

**#4. ARSENAL VS CHELSEA (29/04/23)**

Stamford Bridge imekuwa uwanja wa kuwinda wenye furaha kwa Arsenal ya Arteta na waliwashinda Chelsea kwa mtindo wa kuvutia kabla ya Kombe la Dunia. Ushindi wao wa 1-0 ulikuwa mojawapo ya maonyesho yao ya kuvutia zaidi msimu huu, lakini 'The Blues' wataonekana kutaka kusahihisha makosa ya mechi za nyuma.

**#5. NEWCASTLE VS ARSENAL (06/05/23)**

St. James' Park ndio ilikuwa bakuli mbaya ambapo ndoto ya Arsenal ya kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya ilipoishia msimu uliopita. Arsenal waliwaruhusu Tottenham Hotspur kushinda nafasi ya nne, huku wao wakikataliwa na Newcastle.

The Magpies wanajizatiti kwa nguvu zote za kumaliza katika nafasi nne za juu. Ndio timu pekee ya ndani iliyofunga bao safi dhidi ya Arsenal msimu huu, huku pia wakiwa bado hawajaonja kushindwa kwenye ardhi ya nyumbani.

Huu ni mchezo mgumu sana kwa wanaotarajia ubingwa pale St. James' Park itatikisa na kumbukumbu za Mei 2022 zitakuwa kubwa.

**#6. ARSENAL VS WOLVES (28/05/23)**

Inaweza kufikia siku ya mwisho na ingawa nafasi ya timu yao kileleni kwa sasa ni ya afya, mashabiki wengi wa Arsenal bila shaka watakubali matokeo haya.

Kwa hiyo, mchezo wa nyumbani dhidi ya Wolves unaweza kuwa muhimu sana kwa timu ya Arteta. Hii inaelekea kuwa mbio za ubingwa ambazo huenda vijana wa Julen Lopetegui wanaweza kuwa na sauti kubwa katika kuamua kila mshindi.

Manchester City kwa upande wao, watakuwa ugenini dhidi ya Brentford siku ya mwisho.

## ISIKUPITE

KIUNGO wa Manchester City, Kevin De Bruyne mwenye pasi za mwisho 'assists' 11 huku Lionel Messi (10) na Neymar (10) wote wa PSG pamoja na Randal Kolo Muani (10) kutoka Eintracht Frankfurt, ni wachezaji pekee katika ligi tano bora Ulaya ambao wamefikisha tarakimu mbili za 'assists' msimu huu.



Extra Time

# WACHEZAJI 10 BORA WALIOFUNGA MABAO MENGI TANGU MWAKA 2020

**LONDON,** England

WAKATI mashindano ya mataji yanajaribu mishipa ya mchezaji, soka la ligi ni kuhusu uthabiti. Katika kipindi cha msimu wa kuchosha, wanasoka huwekwa mbele ya timu zilizo na sifa tofauti, uwezo na mitindo tofauti ya kucheza. Ni wale tu walio wakali zaidi na wanaoweza kubadilika zaidi na wataweza kukabiliana na soka la ligi na kutumia mguso wa kuvutia, wiki baada ya wiki.

Leo, tutaangalia baadhi ya washambuliaji bora ambao wamekuwa na kiwango bora cha kuvutia tangu mwaka 2020. Hapo chini kuna wafungaji 10 bora ambao wamefunga mabao mengi zaidi kwenye ligi tangu mwaka 2020, twende sasa...

### #10. LIONEL MESSI - MABAO 56

Mchezaji nyota wa Paris Saint-Germain (PSG), Lionel Messi amefunga mabao 56 katika michezo 96 ya ligi tangu mwaka 2020.

Messi, ambaye aliisaidia Argentina kutwaa Kombe la Dunia la FIFA la 2022 Desemba mwaka jana, alifunga mabao 25 kwenye Ligi Kuu Hispania, LaLiga, msimu wa 2019-20, na kushinda Kiatu cha Dhahabu 'Pichichi Trophy'. Kati ya jumla ya mabao yake, alifunga 12 mwaka 2020.

Katika msimu wa 2020-21, Messi alifunga mabao 30 katika mechi 35 za LaLiga. Barcelona haikushinda taji la Hispania, lakini Messi alishinda tuzo ya Pichichi. Msimu uliofuata, akiwa PSG, Messi alifunga mara sita pekee katika mechi 26 za Ligue 1 huku klabu hiyo ikishinda taji la Ligi Kuu Ufaransa.

Msimu huu, amekuwa mzuri zaidi, tayari amefunga mabao nane na kutoa asisti 10 katika mechi 15.

### #9. WISSAM BEN YEDDER - MABAO 61

Mshambuliaji wa kati wa AS Monaco, Wissam Ben Yedder amefunga mabao 61 katika michezo 100 ya ligi tangu mwaka 2020, akiibuka mfungaji bora wa timu hiyo ya Ufaransa kwenye Ligue 1.

Ben Yedder, aliyejiunga na Monaco Julai 2019, alifunga mabao 18 katika michezo 26 ya Ligue 1 katika msimu wake wa kwanza. Mabao matano kati ya hayo yalikuja katika nusu ya pili ya msimu wa 2019-20. Msimu uliofuata, alifunga mabao 20 katika michezo 37 na kuisaidia Monaco kumaliza katika nafasi ya tatu. Katika msimu wa 2021-22, Ben Yedder alirekodi kurejea kwake kwa mabao 25 katika mechi 37.

Ben Yedder amefurahia mwendo mzuri wa Ligue 1 msimu huu pia, akifunga mara 11 na kutoa asisti mbili katika mechi 16.

### #8. MOHAMED SALAH - MABAO 62

Mshambuliaji wa Liverpool, Mohamed Salah, amefunga mabao 62 katika mechi 108 kwenye soka la Uingereza tangu 2020.

Katika msimu wa 2019-20, Salah alifunga mara 19 katika mechi 34 huku Liverpool ikishinda taji lao la 19 la ligi. Mabao yake kumi kati ya 19 alifunga katika kipindi cha pili cha msimu wa 2019-20, mwaka 2020. Msimu uliofuata, Salah alifunga mara 22 katika mechi 37. Aliboresha idadi yake msimu wa 2021-22, akiingia akiwa na mabao 23 katika michezo 35 huku 'Wekundu' hao wakipoteza mbio za ubingwa kwa Manchester City kwa pointi moja pekee.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Misri msimu huu amefunga mabao saba pekee na kutoa pasi nne za mabao katika mechi 18 alizocheza hadi sasa.

### #7. HARRY KANE - MABAO 62

Mchezaji nyota wa Tottenham Hotspur, Harry Kane amekuwa mmoja wa washambuliaji bora kwenye Ligi Kuu England, huku akifunga mabao 62 katika mechi 101 tangu 2020.

Kane alifunga mabao 18 ya ligi katika mechi 29 msimu wa 2019-20, huku saba kati ya msimu huo akifunga 2020. Msimu uliofuata, alifunga mabao 23 katika michezo 35, akishinda Kiatu cha Dhahabu. Msimu wa 2021-22, Kane alianza polepole, lakini akaongeza kasi katika raundi ya pili na kumaliza na jumla ya mabao 17 katika michezo 37.

Kane ameonekana kuwa mkali zaidi msimu huu, akifunga mara 15 katika mechi 17 kwenye Ligi Kuu England.

### #6. KARIM BENZEMA - MABAO 67

Mshambuliaji nyota wa Real Madrid, Karim Benzema, ameibuka kuwa hirizi ya klabu hiyo katika zama za baada ya Cristiano Ronaldo. Tangu Januari 2020, Mfaransa huyo amefunga mara 67 katika mechi 95 za LaLiga.

Katika msimu wa 2019-20, Benzema alifunga mara 21 na kutoa asisti nane katika michezo 37 huku Real Madrid ikishinda LaLiga. Mabao yake tisa katika msimu wa 2019-20 wa LaLiga alifunga mwaka 2020. Msimu uliofuata, Benzema alifunga mabao 23 na kutoa asisti tisa katika mechi 34 za LaLiga, lakini Madrid walishindwa kutwaa taji, huku Atletico Madrid wakitwaa ubingwa huo.

Msimu wa 2021-22 uliashiria msimu bora zaidi wa kazi ya Benzema. Alifunga mabao 27 na kutoa asisti 12 katika michezo 32 huku 'Los Blancos' hao wakishinda LaLiga. Mchezaji huyo wa zamani wa Kimataifa wa Ufaransa, ameonekana kuwa mkali msimu huu pia, akifunga mara nane na kutoa asisti katika mechi 9 za LaLiga hadi sasa.

### #5. CRISTIANO RONALDO - MABAO 69

Ni nyota wa Al Nassr, Cristiano Ronaldo alifunga mabao 69 katika michezo 93 ya ligi kwenye ligi tano bora za Ulaya kati ya Januari 2020 na Novemba 2023.

Nyota huyo wa Ureno alifunga mabao 31 katika mechi 33 za Serie A msimu wa 2019-20, huku mabao 21 kati ya hayo akifunga katika kipindi cha pili cha msimu, mwaka 2020. Juventus ilishinda taji la Serie A mwaka huo.

Msimu uliofuata, alifunga mabao 29 katika michezo 33, akishinda tuzo ya mfungaji bora, lakini akakosa taji la Serie A. Alijiunga tena na Manchester United msimu uliofuata na kufunga mabao 18 katika mechi 30 kwenye Ligi Kuu England.

Kwa bahati mbaya, mambo yalikwenda tofauti chini ya kocha Erik ten Hag msimu wa 2022-23, huku akiondoka kwenye klabu hiyo Novemba baada ya kufunga bao moja pekee katika mechi 10 za ligi.

### #4. CIRO IMMOBILE - MABAO 73

Mshambuliaji wa Lazio, Ciro Immobile, amekuwa mchezaji anayeongoza Serie A muongo huu, akifunga mabao 73 katika mechi 101 za ligi.

Immobile alishinda tuzo yake ya kwanza ya mfungaji bora katika msimu wa 2019-20, akifunga mara 36 katika michezo 37. Mabao yake 19 ya kuvutia kati ya 36 yalipatikana katika kipindi cha pili cha msimu wa 2019-20.

Msimu uliofuata, matokeo ya Immobile yalishuka sana, huku akifunga mabao 20 katika michezo 35. Msimu uliopita, Immobile alionekana tena kama mfungaji bora akifunga mara 27 katika mechi 31.

Immobile, ambaye kwa sasa anauguza jeraha la misuli ya paja, amefunga mabao saba katika mechi 15 alizocheza msimu huu.

### #3. KYLIAN MBAPPE - MABAO 75

Mshambuliaji wa Paris Saint-Germain, Kylian Mbappe, amekuwa moto sana kuwakabili walinzi wa Ligue 1, huku akifunga mara 75 katika mechi 91 za ligi tangu mwaka 2020.

Katika msimu wa 2019-20, Mbappe alifunga mabao 18 katika mechi 20. Alifunga mabao saba na kutoa asisti mbili katika kipindi cha pili cha msimu wa 2020-21, mwaka 2020. Alishinda tuzo ya mfungaji bora msimu huo.

Katika msimu wa 2020-21 wa Ligue 1, Mbappe alifunga mara 27 katika mechi 31. PSG walikosa taji la ligi, lakini Mbappe alihifadhi tuzo yake ya mfungaji bora. Msimu uliopita, Mbappe alifunga mara 28 katika mechi 35 na kushinda tuzo yake ya mfungaji bora kwa mara ya nne mfululizo na kuiwezesha PSG kutwaa taji la 10 la Ligue 1.

Msimu huu pia, Mbappe amekuwa katika hali nzuri. Akiwa amefunga mara 13 na kutoa pasi mbili za mabao katika mechi 17.

### #2. ERLING HAALAND - MABAO 83

Mshambuliaji wa Manchester City, Erling Haaland, mchezaji mwenye umri mdogo zaidi kwenye orodha hii, amefunga mabao 83 katika mechi 84 za ligi tangu 2020.

Haaland alijiunga na Borussia Dortmund kutoka RB Salzburg Januari 2020. Kati ya Januari na Juni, alifunga mara 13 katika mechi 15. Msimu uliofuata, alitikisa nyavu mara 27 katika mechi 28. Katika msimu wake wa mwisho akiwa Dortmund, Haaland alifunga mara 22 katika mechi 24 za Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga.

Haaland amekuwa katika daraja la aina yake kwenye Ligi Kuu England. Haaland amefunga mara 21 na kutoa asisti tatu katika michezo 17 ya Ligi Kuu England hadi sasa. Ilimchukua mechi 14 pekee kufikia mabao 20. Hakuna mchezaji katika historia aliyefikia hatua hiyo mapema namna hiyo.


### #1. ROBERT LEWANDOWSKI - MABAO 104

Akiwa amefunga mabao 104 katika mechi 92 tangu 2020, mshambuliaji wa Barcelona Robert Lewandowski yuko kileleni mwa orodha hii.

Lewandowski, ambaye alijiunga na Barca kutoka Bayern Munich majira ya joto yaliyopita, alifunga mara 34 msimu wa 2019-20, huku mabao 15 kati ya hayo akifunga 2020. Msimu uliofuata, alipanda daraja, akifunga mabao 41 katika mechi 29 pekee.

Hatimaye, katika msimu wa 2021-22, alifunga mara 35 katika michezo 34. Bayern Munich ilishinda taji la Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, katika misimu yote mitatu, huku Lewandowski akitwaa tuzo ya mfungaji bora katika kila msimu.

Ametikisa nyavu akiwa na Barcelona pia, ambapo hadi sasa anaongoza kwenye orodha ya wafungaji bora akiwa amefunga mabao 13 katika mechi 15 alizocheza.



ERLING HAALAND

## Nukuu

"Cristiano Ronaldo ni ingizo zuri, kwani anasaidia kuwatawanya mabeki. Ni mmoja wa wachezaji bora duniani. Hatamalizia soka lake Al Nassr, atarejea Ulaya. Ronaldo anatarajiwa kurejea Ulaya," **Kocha Mkuu wa Al Nassr, Rudi Garcia.**



"Tena, siwezi kueleza. Lakini hizi dakika 15 haziwezi kuruhusiwa. Inapaswa kubadilika. Hiyo ndiyo ilivyo. Nasimama hapa tena na kwa dakika 15 za kwanza sina maelezo, samahani. Mwishowe, tulipoteza 3-0 kwa sababu bao katika kipindi cha pili labda ndiyo ilikuwa mara yao ya kwanza kuvuka nusu ya mstari. Lakini ni sawa kwa sababu unapoanza hivi hustahili chochote katika mchezo wa Ligi Kuu," **Kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp akiomba msamaha baada ya kipigo cha mabao 3-0 dhidi ya Wolves juzi.**



"Lionel Messi alikuwa injini muhimu sana, kama lengo lake na nafasi alizotengeneza. Ninaomba timu kwa ajili ya Leo kwa kumfanyia kazi. Ni lazima asamehewe baadhi ya majukumu. Wachezaji wenzake lazima waongeze juhudi na kutengeneza mikimbio ya haraka ili apige pasi, ambazo ni nadra sana katika soka la leo, katika nafasi ndogo," **Kocha wa Paris Saint-Germain, Christophe Galtier**



# USAJILI WA DIRISHA DOGO ULIOANZA KULIPA BARA

**Na Adam Fungamwango**

BAADHI ya wachezaji waliosajiliwa kwenye dirisha dogo la usajili Ligi Kuu Tanzania Bara, wameanza kwa kasi kubwa wakizisaidia timu zao kupata ushindi kwenye mechi za ligi hiyo.

Wachezaji hao ambao wamesajiliwa kati ya Desemba 16, mwaka jana na Januari 15, mwaka huu, wameonyesha maana halisi ya ongezeko la wachezaji kwenye dirisha hilo ambalo ni maalum kwa ajili ya kuboresha mapungufu yaliyojitokeza kwenye mechi za mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu.

Hawa hapa ni wachezaji ambao tayari wameonyesha ni kwa nini timu zao hazikufanya makosa kuwasajili kipindi hiki...

**KELVIN SABATO - POLISI TANZANIA**

Alifunga mabao mawili kwenye mechi iliyochezwa Desemba 26, mwaka jana ambapo timu yake ya Polisi Tanzania ilicheza dhidi ya Coastal Union kwenye Uwanja wa Ushirika, Moshi mkoani Kilimanjaro na miamba hiyo kufungana mabao 3-3.

Sabato, straika Mtanzania ambaye ameshapitia timu nyingi za Ligi Kuu Tanzania Bara, alisajiliwa kipindi hiki cha dirisha dogo akitokea Singida Big Stars na kuingia kwenye orodha ya wachezaji walioanza kwa moto kwenye timu zao mpya.

**SAIDO NTIBAZONKIZA - SIMBA**

Saido, raia wa Burundi, alianza kuthibitisha kuwa klabu hiyo haikukosea kumsajili kipindi cha dirisha dogo akitokea Geita Gold, alipopachika mabao matatu 'hat-trick' kwenye mechi dhidi ya Tanzania Prisons iliyochezwa katika Uwanja wa Benjamin Mkapa Desemba 30, mwaka jana, akiiwezesha timu yake kupata ushindi wa mabao 7-1.

Kama vile haitoshi, kiungo huyo mshambuliaji ambaye alishawahi kuichezea Yanga, alifunga mabao mawili kwenye mechi iliyofuata ambayo Simba ilicheza dhidi ya Mbeya City Januari 18 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, timu yake ikishinda mabao 3-2 na Ijumaa iliyopita akafunga tena bao 1 timu yake ikishinda 3-1 dhidi ya Singida Big Stars katika uwanja huo.




Enock Mayala - Polisi Tanzania

Huyu ni straika kutoka Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo. Anaitwa Enock Mayala akisajiliwa kipindi cha dirisha dogo kutoka Sangabalende ya nchini humo, aliifunga timu yake ya Polisi Tanzania mabao mawili, wakati wakishinda mabao 2-0 wakiwa ugenini katika Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa Lindi dhidi ya Namungo, mechi ikipigwa Januari 14.

Ulikuwa ni ushindi muhimu kwa timu hiyo kwani ilikuwa haijafanya hivyo kwa muda mrefu kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

**JEAN BALEKE - SIMBA**

Straika mpya wa Simba, Jean Baleke, ambaye ni raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, alifunga bao lake la kwanza, ikiwa ni mechi ya kwanza tu kucheza akisajiliwa na klabu hiyo kipindi cha dirisha dogo, kutoka klabu ya Nejmeh ya Lebanon.

Mchezaji huyo alikuwa anachezea timu hiyo kwa mkopo kutokea TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo.

Mechi hiyo ilichezwa Januari 22, mwaka huu kwenye Uwanja wa Jamhuri Dodoma na lilikuwa bao pekee kwenye mechi hiyo, kabla ya Ijumaa iliyopita kuziona tena nyavu timu yake ikishinda 3-1 dhidi ya Singida Big Stars katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam naye akawa mmoja wa wachezaji ambao wameanza kulipa.

**ELIUS MAGULI - GEITA GOLD**

Akiwa amejiunga na Geita Gold kipindi cha dirisha dogo, Elius Maguli, staika wa zamani wa Simba na Timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars, Januari 20 mwaka huu, alifunga bao kwenye Uwanja wa Nyankumbu, Geita, timu yake ilipocheza dhidi ya Polisi Tanzania na kuiwezesha kutoka sare ya bao 1-1.

Kabla ya hapo, Januari 14, Maguli, alitoa pasi ya mwisho 'assist' kwa Edmund John aliyefunga bao la pili kwenye mechi ya Ligi Kuu, timu yake ikishinda mabao 2-0 dhidi ya Dodoma Jiji katika uwanja huo huo wa Nyankumbu Geita.

**JE, WAJUA?**



ROBERT Lewandowski, Sergio Busquets wa Barcelona, Pau Torres anayeichezea Villarreal na Inaki Williams wa Athletic Bilbao, ni wachezaji wakubwa na muhimu katika kuziwezesha timu zao kupata ushindi, ambao hawakuwahi kukaa nje ya uwanja kwa sababu ya kuwa majeruhi kwenye mechi za La Liga mwaka 2022.

# Walalamika Jiji kuvunja nyumba bila taarifa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAKAZI wa Mtaa wa Chidachi, Kata ya Mkonze wameulalamikia uongozi wa Jiji la Dodoma kuvunja nyumba zao bila kupewa notisi wala kuwashirikisha viongozi wa serikali yao ya mtaa.

Wakizungumza na waandishi wa habari mmoja wa wakazi hao, Carlos Msendekwa, alisema wanashangaa kuona watumishi wa halmashauri kuvunja nyumba zao bila ya kuwapatia notisi yoyote.

"Leo asubuhi walikuja watu kutoka Jiji wakasema wanakuja kwa ajili ya kupima na kufanya tathmini ya maeneo ili kuanza kugawa viwanja kwa wananchi lakini baada ya kuzunguka nao tulipoondoka tuu tukaambiwa kuwa warudi na kuvunja nyumba pamoja na misingi ambayo ilishaanza kujengwa," alisema Msendekwa.

**Tumechoka kuendelea kuonewa na viongozi wa Jiji, tumetumia gharama kubwa kununua saruji, maji kisha mtu anakuja kuvunja bila sababu yoyote.**

Gradenes Edward, alisema kitendo kilichofanywa na Jiji siyo cha kibinadamu kwa kuwa wamejenga nyumba zao kwa kujinyima na familia zao.

"Hali yenyewe ilivyokuwa ngumu hivi sasa ndugu mwandishi halafu mtu anakuja kukuvunjia tuu bila hata taarifa hata uongozi wa mtaa hawafahamu. Tunamwomba Rais Samia Suluhu Hassan atusaidie kupata haki yetu.

"Tumechoka kuendelea kuonewa na viongozi wa Jiji, tumetumia gharama kubwa kununua saruji, maji kisha mtu anakuja kuvunja bila sababu yoyote," alisema.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Chidachi, Mhamed Ramadhan, alisema eneo hilo maarufu kwa jina la Upendo limekuwa na mgogoro wa muda mrefu baina ya Jiji la Dodoma na wananchi.

"Jiji walichukua hili eneo ili wapime viwanja na upimaji ulishafanyika toka Ijumaa na kuhakiki eneo hili na hata leo (juzi) asubuhi tuliendelea na upimaji huo lakini baada ya mimi kuondoka na tu nilipigiwa simu kuwa watu wa Jiji wanavunja na nilipokuja nikakuta misingi mitatu ivunjwa na maboma mawili," alisema.

Alisema walipohoji kwa Ofisa Mipango Miji alisema wamevunja kwa sababu wananchi hao wamejenga wakati wataalamu wa Jiji walipokuwa wakifanya uhakiki.

"Mimi kama kiongozi wa mtaa huu ushauri kwa Mkurugenzi wa Jiji namuomba kutushirikisha katika hili ili lifike mwisho kwani imekuwa muda sasa eneo hili kuwa na mgogoro na Jiji la Dodoma,"alisema Ramadhan.

Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Joseph Mafuru, alipoulizwa kuhusu malalamiko ya wananchi hao, alidai kuwa hilo ni eneo la serikali na wamevunja nyumba hizo kutokana na wananchi kuwahi kujenga ili Jiji watakapokuja ionekane kuwa walikuwapo muda mrefu.

"Hilo ni eneo la serikali na tumevunja nyumba chache za wananchi waliowahi kujenga na kesho tunakwenda kuendelea kuvunja nyingine,"alisema Mafuru.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, Abdallah Chaurembo, akiwasilisha taarifa ya kamati hiyo bungeni mwishoni mwa wiki alisema kutokana migogoro mingi ya ardhi katika Jiji la Dodoma, Bunge linaiagiza serikali kufanya uchunguzi wa kina ili kubaini chanzo na kuchukua hatua.

Alisema: "Bunge linaiagiza serikali ifanye uchunguzi wa kina ili kubaini chanzo cha migogoro ya ardhi Dodoma na kuchukua hatua stahiki kama itabainika kuwa kuna mtu ameonewa basi apatiwe haki yake," alisisitiza Chaurembo.

## Serikali: Hatutawazuia wakulima kuuza mazao yao nje

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imesema haitofunga mipaka wala kumzuia mkulima kuuza mazao yake nje kwa kisingizio cha kudhibiti mfumuko wa bei ya vyakula hapa nchini.

Aidha, serikali imesema imejipanga kuongeza kununua chakula ikiwamo kuhifadhi, ili kuweza kukabiliana na bei ya vyakula pale itakapopanda katika maeneo mbalimbali.

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, aliyasema hayo juzi kwenye mkutano wa kisheria na kisera kwenye uzalishaji na uuzaji wa zao la tumbaku jijini hapo.

Bashe alisema serikali imewekeza nguvu nyingi katika sekta ya kilimo ili kuhakikisha wakulima wanalima kilimo chenye tija badala ya kuwazuia kuuza mazao yao.

Alisema uwekezaji unaofanywa kwenye kilimo lengo lake sekta hiyo ikue kiuchumi na kuongeza pato la taifa.

"Wakati sasa umefika kwa mkulima kunufaika na kilimo kutokana na kazi kubwa anayofanya hivyo ni muhimu sasa akaachiwa ajipangie bei mwenyewe Ili kukua kiuchumi," alisema Bashe.

Pia aliwataka wakuu wa mikoa na wilaya kuwasaidia wakulima kuongeza tija kwenye kilimo ili wazidi kuzalisha kuongeza na kuhifadhi mazao ya chakula ambayo yatasaidia hapo baadaye.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Dk. Christine Ishengoma, aliwataka wananchi kujikita kwenye kanuni bora za kilimo ili waweze kuendesha kilimo chenye tija ambacho kitawapa mazao mengi.



Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri, akipanda mti kwenye eneo la Bonde la Wami Ruvu Dodoma Hifadhi ya Makutupora mwisho wa wiki, wengine ni wafanyakazi wa bonde hilo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Uongozi Bonde la Maji watakiwa kuwatumia vijana kwenye ulinzi

**Na Ibrahim joseph,** DODOMA

UONGOZI wa Bonde la Maji la Wami Ruvu Dodoma wametakiwa kuacha kutumia nguvu katika ulinzi bali washirikishe vikundi vya vijana ili kuimarisha ulinzi wa maeneo yaliyohifadhiwa.

Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri, alitoa kauli hiyo wakati wa upandaji miti kwenye bonde hilo eneo la Makutupora.

Shekimweri aliwataka uongozi wa bonde hilo kuvitumia vikundi vya vijana vilivyoko kwenye maeneo ya hifadhi ili kuimarisha ulinzi kwenye maeneo hayo.

"Acheni kutumia nguvu kubwa katika ulinzi wa maeneo ya uhifadhi, vipatieni misaada vikundi vya vijana kwa kuwapa miradi ya mizinga ya nyuki ili kusaidia ulinzi,"alisema.

Alisema wanaweza kuwasaidia miradi ya ufugaji nyuki kuzunguka eneo la hifadhi hiyo ili kusaidia ulinzi wa watu wanaovamia na kufanya shughuli za uzalishaji uchumi ndani ya hifadhi.

Alibainisha kuwa badala ya kutumia fedha nyingi kuweka mafuta na kuwalipa askari kwa ajili ya doria za eneo la uhifadhi wa bonde hilo na maeneo mengine nchini watumie mbinu hiyo itasaidia.

Hivyo, aliwataka kuwapa vijana mizinga ya nyuki ambayo itakuwa ikiwafanya kupeana zamu ya kulinda dhidi ya wavamizi wa eneo lililohifadhiwa.

Aidha, alisema kwa wale wanaoendelea kuingiza mifugo yao kwenye eneo hilo wanastahili kukamatwa na kuchukuliwa hatua za kisheria.

Aliongeza kuwa eneo hilo la bonde ni chanzo kikuu cha maji kwa ajili ya Jiji la Dodoma, hivyo kunatakiwa kulindwa ili kuimarisha huduma ya maji kwa wakazi wa Jiji hilo.

Mkurugenzi wa Bodi ya Maji Bonde la Wami Ruvu Dodoma, Felisiana Mpanda, alisema wanakabiliwa na matatizo ya wananchi kuvamia eneo la hifadhi la bonde hilo.

Mpanda alisema wananchi hao wamekuwa wakiingia eneo la hifadhi na kufanya shughuli za kilimo pamoja na kuingiza mifugo yao eneo hilo la hifadhi.

Mpanda alisema kuwa baadhi ya wananchi wamekuwa wakiingia eneo la hifadhi na kukata miti kwa ajili ya kuchoma mikaa na pamoja na kutumia miti hiyo kama kuni.

Aidha, Mpanda alisema bodi hiyo imekusudia kupanda miti 10,000 katika msimu huu wa mvua ili kulinda hifadhi hiyo.

Mpanda alisema hadi kufikia mwisho wa wiki hii wameshapanda miti zaidi ya 6,000 na wanaishirikisha jamii katika kupanda miti.

Pia alisema wamekuwa wakitoa elimu kwa wananchi wa vijiji vinavyozunguka bonde hiyo ili kulinda vyanzo hivyo muhimu vya maji kwa watu wengi.





# Waliofeli darasa la saba kujiunga vyuo vya ufundi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANAFUNZI zaidi ya 3,000 waliofeli mitihani ya darasa la saba mwaka jana mkoani Mbeya na kukosa sifa za kuendelea na masomo ya sekondari, wanatarajiwa kujiunga na vyuo mbalimbali vya ufundi ili wapate ujuzi utakaowasaidia kujiajiri.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu maendeleo ya sekta ya elimu katika mkoa huo.

Alisema serikali ya mkoa huo imeanzisha utaratibu huo ili kuepusha ndoto za watoto hao kufa na wao kugeuka kuwa watoto wa mtaani na wasiokuwa na ajira zenye staha kutokana na kutokuwa na ujuzi wa aina yoyote.

Alisema vijana hao watajiunga na vyuo mbalimbali vikiwamo vya ufundi stadi, vyuo vya maendeleo ya jamii na wengine watajiunga na elimu ya watu wazima na kwamba kila mwanafunzi atachagua kile anachotaka kusomea.

**Kila chuo kina mtaala wake tofauti na kingine kulingana na aina ya mafunzo yanayotolewa hasa vyuo vya ufundi na vyuo vya maendeleo ya jamii.**

Homera alisema lengo la serikali ni kuzalisha mafundi wengi ambao watasaidia kwenye utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo katika mkoa huo pamoja na kupunguza tatizo la ukosefu wa ajira kwa vijana.

Alisema mafunzo watakayokuwa wanayapata vijana hao yatakuwa yenye gharama nafuu kulingana na chuo ambacho mwanafunzi husika atachaguliwa kwenda kusoma.

Alisema mpaka sasa tayari watoto hao wamepangwa kwenye vyuo hivyo katika kila wilaya ya mkoa huo na wazazi wataendelea kuhamasishwa ili washirikiane na serikali kwenye uendeshaji wa mafunzo hayo.

"Fedha watakazokuwa wanalipa wazazi sio kama ada bali ni gharama kwa ajili ya chakula kwa wanafunzi wenyewe lakini na kununulia baadhi ya vifaa kwa ajili ya kuwafundishia na hili ni wazo la mkoa wetu ambalo tumebuni wenyewe," alisema Homera.

Alisema baada ya vijana hao kuhitimu mafunzo hayo watajiunga kwenye vikundi mbalimbali ili wapatiwe mikopo ya asilimia 10 za mapato ya ndani ya halmashauri kwa ajili ya kupata mtaji wa kuendeshea shughuli zao.

Hivyo, aliwataka viongozi wa wilaya na kata kushirikiana kuhamasisha wazazi kuwapeleka watoto wao kwenye vyuo hivyo na kuchangia gharama ili kuwasaidia kupata ujuzi utakaowasaidia kuendesha maisha yao ya baadaye.

Ofisa Elimu wa Mkoa wa Mbeya, Mwalimu Ernest Hinju, alisema wanafunzi hao watapata mafunzo kwa kuzingatia mitaala ya kila chuo watakachopangiwa na kwamba tayari miongozo ya utoaji wa mafunzo hayo ipo.

Alisema kila chuo kina mtaala wake tofauti na kingine kulingana na aina ya mafunzo yanayotolewa hasa vyuo vya ufundi na vyuo vya maendeleo ya jamii.

Alisema kupitia ujuzi watakaoupata vijana hao watakuwa na uwezo wa kujipatia kipato kitakachosaidia kukuza uchumi wao, uchumi wa Mkoa wa Mbeya na taifa.



Wakazi wa Kijiji cha Itamboleo wilayani Mbarali Mkoa wa Mbeya, wakishiriki kupanda miti eneo la ardhi oevu lenye ukubwa wa ekari 10 mwishoni mwa wiki kwa lengo la kutunza chanzo cha maji kilichoko eneo hilo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Viongozi CCM wapewa miezi mitatu kuhamisha ofisi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

VIONGOZI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Mbeya Vijijini wamepewa miezi mitatu kuhamisha ofisi katika Wilaya ya Mbeya Mjini ili kusogeza huduma kwa wananchi.

Agizo hilo lilitolewa juzi na Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Mbeya, Dk. Stephene Mwakajumilo, wakati wa maadhimisho ya miaka 46 ya chama hicho yaliyofanyika katika Kijiji cha Zyila wilayani humo.

Alisema kitendo cha ofisi za wilaya hiyo kuwa katika wilaya nyingine ni kuwakosesha huduma wananchi wa wilaya hiyo jambo ambalo siyo lengo la CCM.

Hivyo aliwataka kama hawana majengo ya kuhamia wajenge ofisi zao haraka na kuhamia, huku akisisitiza kuwa endapo hawatatekeleza hatua zitachukuliwa ili iwe fundisho.

Alisema lengo la chama hicho ni kuhakikisha kinakuwa karibu na wananchi kwa kuhakikisha kinawahudumia kwa ukaribu badala ya kujiweka mbali.

Dk. Mkwajumulo aliwataka wananchi wa Wilaya ya Mbeya kuendelea kukiamini chama hicho kwa maelezo kuwa ndicho chama pekee chenye mwelekeo wa kuleta maendeleo katika nchi.

Alisema kwa sasa nchi inapata maendeleo makubwa kutokana na utekelezaji wa Ilani ya chama hicho tawala.

**Kitendo cha ofisi za wilaya hiyo kuwa katika wilaya nyingine ni kuwakosesha huduma wananchi wa wilaya hiyo jambo ambalo siyo lengo la CCM.**

# H'shauri yazalisha miche ya michikichi, yawapa wakulima

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya, imezalisha miche 33,000 ya michikichi na kuigawa kwa wakulima wilayani humo ikiwa ni sehemu ya mikakati ya kuimarisha kilimo cha zao hilo.

Aidha, halmashauri hiyo imeanzisha mkakati huo ili kukuza kipato cha wananchi na kukabiliana na tatizo la uhaba wa mafuta ya kupikia ambao umekuwa ukilikabili taifa na kusababisha bei ya bidhaa hiyo kuwa ya juu.

Miche hiyo imeandaliwa kwa ushirikiano kati ya halmashauri hiyo na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI) Naliendele ambayo imekuwa ikisaidia masuala ya utaalamu kwenye uzalishaji wa miche hiyo ili iendane na mazingira.

Akizungumza mwishoni mwa wiki wakati wa kugawa baadhi ya miche hiyo kwa wakulima, Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, Kenneth Izirano, alisema miche iliyoandaliwa inatosha kupandwa kwenye mashamba yenye ukubwa wa ekari 674.2.

"Miche hii itakuwa inapandwa kitaalamu na kwa mujibu wa wataalamu ni kwamba kila ekari moja itakuwa na miche 50, ni miche ambayo inaanza kuzaa mapema na hivyo tunaamini kwamba kipato cha wakulima wetu kitaongezeka na hata pato la halmashauri litakua," alisema Izrano.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, Katule Kingamkono, alisema lengo la halmashauri ni kuhakikisha ifikapo mwaka 2025 wananchi wawe wamepanda zaidi ya miche 500,000 ya michikichi.

Alisema wanaigawa miche hiyo bure ili kuwahamasisha zaidi wananchi kulima kwa maelezo kuwa katika miaka ya karibuni kilimo cha zao hilo kimekuwa kikipuuzwa na baadhi ya wakulima.

Alisema zao hilo ni miongoni mwa ubunifu wa halmashauri kupata vyanzo vipya vya mapato kwa miaka ijayo akisisitiza kuwa itakapoanza kuzaa watakusanya mapato yatokanayo na mauzo.

Baadhi ya wakulima walisema miche ya kisasa wanayopewa itawasaidia kuondokana na umaskini kutokana na kuongeza kiwango cha uzalishaji wa zao hilo.

Mmoja wa wakulima hao, Aden Kajela alisema kwenye zao hilo wanapata faida kutokana na kila kitu kuwa na soko ambavyo ni mafuta, malighafi kwa ajili ya kuzalisha sabuni hasa mbegu pamoja na maganda ambayo yanatumika kutandaza nyumbani ili kuondoa tope.

Mkuu wa Wilaya ya Kyela, Josephine Manase, aliagiza miche hiyo pia kugawiwa kwenye taasisi za umma ili kuongeza tija ya uzalishaji wa zao hilo badala ya kuwapatia wakulima pekee.

Aliagiza miche hiyo kugawiwa pia kwenye shule za msingi na sekondari ili nazo zipande kwa ajili ya kufundishia wanafunzi na kupata kipato kitakachotokana na zao hilo.

Pia alisisitiza kilimo cha zao hilo kuanza kurithishwa kwa watoto tangu wakiwa wadogo ili wafahamu namna ya kuzalisha na manufaa yake.





# Wahadharishwa uchimbaji kwenye maeneo ya Mji Mkongwe

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKURUGENZI Mkuu wa Mamlaka ya Mji Mkongwe, Ali Said Bakari, amewataka wananchi wanapotaka kuchimba katika maeneo ya Mji Mkongwe wafuate utaratibu wa kupatiwa kibali.

Alitoa angalizo hilo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusiana na tukio la uchimbaji wa shimo la maji taka ambalo lilikutwa na mabaki ya mifupa ya binadamu pamoja na masalia ya vitu mbalimbali vya thamani.

Alisema kupewa ridhaa na mamlaka yeyote kufanya kitu chochote cha maendeleo katika Mji Mkongwe bila kupatiwa kibali ni kosa kisheria.

Naye Mkurugenzi wa Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale Zanzibar, Mariam Mohamed Mansab, alisema shughuli zozote zinazohusiana na uchimbaji kwa Zanzibar ni vyema kuhusishwa na Idara ya Mambo ya Kale.

Aidha, alifahamisha kuwa jambo hilo kutokezea bila ya kupatiwa taarifa mapema imeharibu utafiti ambao ungesaidia kuifahamu historia ya Zanzibar.

"Wananchi mngetoa taarifa mapema kwa Mamlaka ya Mji Mkongwe kungesaidia kufanyika utafiti kujua sehemu hiyo ilikuwa ya kitu gani," alisema.

Naye Ofisa wa Mambo ya Kale, Faki Othman Haji (pichani chini), alisema katika shughuli mbalimbali za utafiti alizofanya hajawahi kuona chungu kilichofinyangwa kwa jiwe na kuwekwa urembo.

Akizungumzia kuonekana kwa mabaki ya binadamu alisema historia inaonesha kuwa kabla ya kujengwa kwa Mji Mkongwe eneo hilo lote lilikuwa makaburi.

Alisema kuwa wananchi wanahitaji kupatiwa elimu ili kufahamu taratibu zilizoko katika Mji Mkongwe iwapo watafanya shughuli zozote za kimaendeleo ikiwamo uchimbaji kuwasiliana na mamlaka husika.



**Wananchi wanahitaji kupatiwa elimu ili kufahamu taratibu zilizoko katika Mji Mkongwe iwapo watafanya shughuli zozote za kimaendeleo ikiwamo uchimbaji kuwasiliana na mamlaka husika.**

# Mufti Zanzibar awataka wazazi kukemea viashiria vya ushoga

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

OFISI ya Mufti ya Zanzibar imewataka wazazi kukemea uhamasishaji wa matukio ya ushoga ambayo yanakwenda kinyume na mafundisho ya dini zote, mila na silka za tabia za Watanzania.

**Vitendo vya ushoga havikubaliki katika jamii lakini vimelaaniwa na Mwenyezi Mungu na watu wanaofanya matukio hao hawana nafasi mbele ya jamii.**

Katibu wa Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar, Sheikh Khalid Ali Mfaume, alitoa wito huo wakati akizungumza na waumini wa dini ya Kiislamu visiwani Zanzibar.

Alisema vitendo vya ushoga havikubaliki katika jamii lakini vimelaaniwa na Mwenyezi Mungu na watu wanaofanya matukio hao hawana nafasi mbele ya jamii.

Alisema yamekuwapo matukio ya kuhamasisha mwenendo wa vitendo hivyo ambavyo vinafanywa na watu mbalimbali wa ndani ya nchi pamoja na msukumo wa kimataifa.

Shekhe Mfaume alisema madhara ya matukio ya vitendo vya ushoga yanafahamika katika jamii ikiwamo taifa kupoteza nguvu kazi ambayo ni tegemeo kwa ajili ya uzalishaji na kuongoza nchi.


"Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar tunakemea vikali kwa nguvu zote matukio yanayokwenda sambamba na kuhamasisha ushoga kwa jamii yetu mambo ambayo hayakubaliki kwa mujibu wa sheria," alisema.

Aidha, aliwataka wazazi kufuatilia mwenendo mzima wa tabia za watoto wao pamoja na kufahamu makundi wanayofuatana nayo na marafiki.

"Wazazi tunatakiwa tuwe macho kufuatilia mwenendo wa tabia za watoto wetu ikiwamo kujifahamu makundi na marafiki zao kwa sababu imebainika kwamba yapo makundi yanayofanya ushawishi mkubwa wa kuwarubuni watoto na kuiga matukio ya ushoga," alisema.

Katibu wa Msikiti Muembe Shauri Unguja, Iddi Shaaban Seif, alisema wamejipanga kuhakikisha wanazitumia nyumba za ibada kama jukwaa la kutoa elimu ya vitendo vya udhalilishaji na athari zake ikiwamo tishio la ushoga.

Alisema: "Msikiti wetu tumekuwa tukiitumia fursa iliyoko ya kutoa hotuba zenye mafundisho ya athari za matukio ya vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia ambapo suala la tishio la ushoga tunalizungumza kwa ajili ya watoto wetu."



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akiwa na mkewe Mariam Mwinyi, katika mazungumzo na msanii wa kizazi kipya (Bongo Fleva), Mbwana Yussuf Kilungi (Mboso), Ikulu jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# SMZ yaridhishwa ushirikiano wa Saudi Arabia kuhusu Hijja

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, amesema Serikali ya Zanzibar imeridhishwa na kazi inayofanywa na nchi ya Saudi Arabia katika kusaidia maendeleo ya kiuchumi na kurahisisha safari za ibada ya Hijja.

Aliyasema hayo juzi alipofanya mazungumzo na Waziri wa Hijja na Umra wa Saudi Arabia, Dk. Abdulfatah Suliman, wakati alipotembelea Mji wa Makka kwa ajili ya kutekeleza ibada ya Umra nchini humo.

Katika mazungumzo hayo, ambayo yalihudhuriwa na Balozi wa Tanzania nchini Saudi Arabia, Balozi Ali Jabir Mwadini, alisema kwamba Serikali ya Zanzibar inathamini ushirikiano ulioko baina ya pande mbili hizo.

Alieleza kwamba wananchi wa Zanzibar wanafarijika na juhudi zinazofanywa na Serikali ya Saudi Arabia katika kukamilisha hatua za kufungua akaunti maalumu ya Hijja ambayo itatumiwa na Mahujaji wa Zanzibar kwa ajili ya matayarisho ya safari ya Hijja.

Alisema akaunti hiyo itasaidia kuondoa matatizo yanayojitokeza katika suala la malipo na kushughulikia miamala mingine muhimu ya kifedha kwa Mahujaji wa Zanzibar.

Aidha, Waziri Haroun alizipongeza taasisi za dini za Saud Arabia kwa kushirikiana na taasisi za Zanzibar katika usafirishaji na usambazaji wa misaada mbalimbali inayotolewa kwa wananchi wa Zanzibar.

Alisisitiza umuhimu wa kuanzisha safari za ndege za moja kwa moja baina ya Saudi Arabia na Zanzibar kwa lengo la kuimarisha biashara, utalii pamoja na kurahisisha usafiri hasa kwa mahujaji na waumini wanaosafiri kwenda Saudi Arabia kwa ajili ya kutekeleza ibada ya Ummra.

Waziri wa Hijja na Umra, Dk. Abdulfattah Suliman Mashat, alisema nchi hiyo inafanya juhudi mbalimbali katika kuhakikisha uhusiano wa kihistoria ulioko baina ya Zanzibar na Saudi Arabia unaimarishwa na kuendelezwa katika sekta mbalimbali zikiwamo elimu, ujenzi wa miundombinu pamoja na usafirishaji.

Aliahidi kulifuatilia ombi la kuanzishwa usafiri wa moja kwa moja kati ya Saudi Arabia na Zanzibar ili kuimarisha na kuongeza kasi ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii ya pande zote mbili.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



117264602

**PASKALINA ERASTO MIYUNGA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye Index No. **S4465-0010** kilichotolewa na Baraza la Mitihani kupitia **QUEEN MARY'S SECONDARY SCHOOL** mwaka 2015. Yeyote atakaekiona atoe taarifa Kituo chochote cha Polisi. TAARIFA YA POLISI: **DOD/CHA/RB/48016/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**RUHUWIKO HUNT CLUB** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 975 BUP – FORD RANGER.** Chassis namba **AFATXXMJ2TAR00242.** Engine namba**WEAT1145516.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/URA/RB/48944/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**TGS CO LTD**

Kampuni ya **TGS CO LTD** inatangaza kupotelewa kwa kadi ya gari aina ya **SCANIA** yenye usajili wa namba **T 594 ALS.** Kwa yeyote atakaeiona au kuokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilicho karibu. **DSM/PHQ/RB/47375/2023.**

## KUFUNGWA KWA KAMPUNI

**MUS ELIYA IBRAHIM MWENYEKITI** wa Kampuni ya **BUSAMBARA COMPANY LIMITED** na baadae ilibadilishwa na kuwa **BWOODO GENERAL AND COMPANY LIMITED**, yenye Namba ya Usajili **155476443** ya tarehe **22 March 2022** wanapenda kuutangazia Umma kuwa kampuni yao imekuwa haifanyi kazi vizuri toka kuanzishwa kwake , hivyo kuamua kuifunga kwa mujibu wa Sheria ya Makampuni - (Brela) - Sura 212.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya TEMEKE**
**Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM**
**Usimamizi wa mirathi Na 75/ 2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU SECILIUS FUSSI**
**KATIKA SHAURI LA MAOMB YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA HAPPINESS SECILIUS FUSSI**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa mirathi mahakama za mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 14 Mwezi 02 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

Endapo kuna yoyote mwenyewe wosia wa marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa

- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

**Imetolewa leo tarehe 18 mwezi 01 mwaka 2023**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**(UNDER CAP. 117, R.E. 2002)**
**The Registration of Documents Acts**
**DEED POLL CHANGE OF NAME**

By this deed I, **GODVICTA SHANGWEEL URIO** of **ARUMERU DISTRICT** wholly absolutly and utterly renounce , relinguish and abandon the use of my former name of **GODVICTOR SHANGWEELI URIOH**, and adopt as from the date of this poll and in substitution of my former name, the name of **GODVICTA SHANGWEEL URIO**

For the purpose of evidence of such determination I herby declare that I shall at all the time hereafter in all records, deeds documents and other writing and in all actions, suits and proceedings as well as in all public and private dealing and transactions and occasions , whatsoever use and subscribe the said name of **GODVICTOR SHANGWEELI URIOH** as my name lieu of and substition for my former name **GODVICTA SHANGWEEL URIO.**

The reason of changing my names is that the name that appears in my National Identity Card is **GODVICTOR SHANGWEELI URIOH,** which appear difference from the name which **GODVICTA SHANGWEEL URIO,** appear in my leaving certificate and form IV Certificate is **GODVICTA SHANGWEEL URIO**

I hereby express authorize and require all and every person and whosoever at all times after date hereof do designate, describe and adress me by name of **GODVICTOR SHANGWEEL URIO.**

**IN WITNESS WHEREOF I** herein substute my old name of **GODVICTOR SHANGWEELI URIOH**, by the new name of **GODVICTA SHANGWEEL URIO,** and have set my hand at **ARUSHA**



## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**TUHERIY GEPSON MAWALLA** anatangaza kupoteza kadi ya gari yenye usajili wa **T 734 ASN CHASISS NO: CWGE24415917 ENGINE NO: QD32109418** Kwa yeyote atakayeziona atoe taarifa polisi. Ametoa taarifa polisi na kupewa namba **ARU/ARU/RB/46766/2023.**


***OFISI ZA MATANGAZO***
***Mikocheni Industial Area, Po.Box 31042, Dar es Salaam.***
***Mobile: +255 - 745 700 710.***
***E-mail: advertise@guardian.co.tz,***
***Website: www.ippmedia.com***

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701***

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Russia yaunganisha maeneo ya Ukraine

**MOSCOW, Russia**

RIPOTI ya kijasusi ya kila siku ya Wizara ya Ulinzi ya Uingereza imesema Russia imeyaunganisha rasmi maeneo inayoyakalia kimabavu ya Ukraine katika Wilaya ya Kijeshi ya Kusini mwa nchi hiyo.

Shirika hilo lilisema habari za kuunganishwa huko zinatokana na ripoti ya Tass kwamba mikoa ya Donetsk, Luhansk, Zaporizhzhia na Kherson, imewekwa chini ya usimamizi wa kamandi ya kijeshi ya nyota tatu iliyoko Rostov-on-Do.

Ripoti hiyo ilisema, hatua hiyo haina uwezekano wa kuwa na athari za haraka katika uvamizi wa Russia nchini Ukraine.

Hata hivyo, kundi la nchi saba zilizoendelea kiviwanda duniani zilikubaliana mwishoni mwa juma lililopita, juu ya ukomo wa bei ya usafirishaji wa mafuta yaliyosafishwa ya Russia.

Waziri wa Fedha wa Marekani, Janet Yellen, alisema katika taarifa yake kwamba makubaliano hayo yanafuata kikomo sawa cha bei kwa mauzo ya mafuta ghafi ya Russia kilichowekwa mwezi Desemba na kusaidia kuendeleza malengo yao ya kuzuia kitu kikuu kinachoingiza mapato ya Russia katika kufadhili vita vyake haramu nchini Ukraine.

***VOA***



Kiongozi wa Kanisa Katoliki Duniani, Papa Francis (katikati), akiwa na Rais wa Burkina Faso, Salva Kiir (wa pili kulia) na viongozi wengine wa kanisa, Ikulu ya Juba juzi. **PICHA: REUTERS**

# Papa Francis ahimiza amani Sudan Kusini

**JUBA, Sudan Kusini**

KIONGOZI wa Kanisa Katoliki Duniani, Papa Francis, ametoa wito kwa viongozi wa Sudan Kusini akiwataka kutafuta amani ya kudumu na kukomesha mateso yanayowakumba raia nchini humo.

Papa Francis aliyewasili nchini Sudan Kusini Ijumaa alasiri akitokea Kongo, alifanya mazungumzo na Rais Salva Kiir wa nchi hiyo jana, huku agenda yake kuu ikiwa ni kusisitiza amani.

Pia aliwahimiza viongozi wa taifa hilo changa kupambana bila kuchoka kusaka amani na kumaliza machafuko nchini humo yanayosababisha madhila ya kila siku kwa raia.

"Hakuna tena nafasi ya kufanywa uharibifu na badala yake taifa lienze kazi hivi sasa ya kujijenga, shirikianeni kukomesha umwagikaji damu, machafuko na uhasama," alisema.

Rais Kiir alikuwa pamoja na hasimu wake wa muda mrefu ambaye ni makamu wa rais wa nchi hiyo, Riek Machar wakati alipomkaribisha Papa Francis kwenye bustani ya ikulu ya rais mjini Juba.

Kwenye mazungumzo na viongozi hao Papa Francis alipendekeza njia mpya ya kuharakisha mchakato wa maridhiano, ikiwamo kuzuia kuingizwa kwa silaha nchini Sudan Kusini, akisema taifa hilo linahitaji vingi vya muhimu badala ya zana za maangamizi.

Pia alipigia upatu umuhimu wa kuimarishwa kwa sera za afya na miundombini ya taifa hilo, huku Sudan Kusini mara kadhaa ikiorodheshwa kuwa moja ya mataifa masikini zaidi ulimwenguni.

Miaka kadhaa ya vita vya wenyewe kwa wenyewe imewaacha raia wake katika hali ngumu ya maisha huku wakikosa huduma za msingi za jamii.

Rais Kiir aliahidi kuanzisha tena mazungumzo ya mjini Roma pamoja na makundi ya waasi ambao hawautambui mkataba wa amani uliotiwa saini na kwamba anatumai wabunge wa nchi hiyo kutoka upande wa upinzani watamuunga mkono kufanikisha upatikanaji amani.

Kuelekea ziara ya kiongozi huyo wa kidini, raia nchini Sudan Kusini walikuwa na matumaini makubwa kuwa kiongozi huyo wa kiroho atasaidia kupunguza mivutano inayolighubika taifa hilo.

Katibu wa Baraza la Makanisa nchini Sudan Kusini, James Latansio, alisema anatamani ziara hiyo iwe mwanzo wa amani na utulivu katika taifa hilo.

Kwenye ziara hiyo Papa Francis amefuatana na Askofu Mkuu wa Canterbury na mkuu wa kanisa la Anglikana Justin Welby na kiongozi wa kanisa la Scotland Iain Greenshields.

***DW***

## Sankara kuzikwa kiheshima Februari 2023

**OUAGADOUGOU, Burkina Faso**

MSEMAJI wa serikali ya Burkina Faso amesema kuwa mwili wa rais wa zamani wa Burkina Faso, Thomas Sankara na wenzake 12 waliouawa Oktoba 15, 1987, hivi karibuni utazikwa mahali walipouawa huko Ouagadougou.

Msemaji huyo ambaye ni Waziri wa Mawasiliano, Jean Emmanuel, katika taarifa aliyoitoa mwishoni mwa juma lililopita, alisema mazishi hayo yatafanyika mwezi huu huko Ouagadougou kwenye eneo la Kumbukumbu ya Thomas Sankara lililotengwa mahali alipouawa.

Alibainisha kwamba baada ya kesi ya wauaji wao 2021-2022, watapaswa kuzikwa kwa heshima na kwamba mwili wa Thomas Sankara na wenzake 12 ilizikwa kwa mara ya kwanza kwenye makaburi yanayopatikana nje kidogo ya mji wa Ouagadougou, Mei 25, 2015 kwa madhumuni ya taratibu za kisheria.

"Mazishi yao mapya yatafanyika kulingana na taratibu za kitamaduni za mazishi na kufuatiwa na sherehe za kidini na kijeshi, pia sherehe ya kitaifa na kimataifa ya kuwaenzi wahanga hao itaandaliwa Oktoba 15, 2023, kwa kuheshimu kumbukumbu zao," alisema.

Thomas Sankara ambaye aliingia madarakani kwa mapinduzi ya kijeshi Agosti 1983, aliuawa Oktoba 15, 1987 wakati wa mapinduzi yaliyochochewa na Blaise Compaore aliyekuwa naibu wake na kwamba Compaore alibaki madarakani hadi maandamano ya kiraia ambayo yalisababisha kuanguka kwake 2014.

Katika kipindi chote cha miaka 27 ya Compaoré madarakani, kifo cha Thomas Sankara, ambaye alitaka kuondoa ukoloni mawazo na kuvuruga utaratibu wa dunia kwa kutetea maskini na wanaokandamizwa, lilikuwa suala la mwiko.

Mwezi Aprili, mahakama ya kijeshi ya Ouagadougou ilimhukumu Compaoré ambaye hayupo, kifungo cha maisha jela kwa jukumu lake katika mauaji ya Thomas Sankara na wenzake 12, kutokana na kesi iliyodumu kwa miezi sita.

***RFI***

**Thomas Sankara ambaye aliingia madarakani kwa mapinduzi ya kijeshi Agosti 1983, aliuawa Oktoba 15, 1987 wakati wa mapinduzi yaliyochochewa na Blaise Compaore aliyekuwa naibu wake na kwamba Compaore alibaki madarakani hadi maandamano ya kiraia ambayo yalisababisha kuanguka kwake 2014.**

# KIDUNDA, TONY ULINGONI SIKU MOJA KUWANIA MKANDA ABU

**Na Saada Akida**

BONDIA wa Ngumi za Kulipwa nchini, Tony Rashid, atapanda ulingoni kutetea mkanda wake wa ubingwa wa Afrika dhidi ya Sabelo Ngebinyana raia wa Afrika Kusini siku ambayo Seleman Kidunda naye atavaana na Patrick Mukala kutoka DR Congo.

Tony atapanda ulingoni kwenye pambano hilo la kimataifa litakalopigwa Februari 24, mwaka huu katika Ukumbi wa Ubungo Plaza, Dar es Salaam.

Tony ana rekodi ya kucheza jumla ya mapambano 18 akiwa ameshinda 14 kati hayo kumi yakiwa ni kwa KO huku akipoteza mawili, moja kwa KO na kutoka sare mara mbili tu.

Mpinzani wake, Sabelo yeye amecheza mapambano 21 kati ya hayo ameshinda 15 ambapo 11 ni kwa KO na amepoteza mapambano sita huku moja likiwa ni kwa KO.

Akizungumza na gazeti hili jana, Tony, alisema anaendelea na mazoezi kwa ajili ya kukabiliana na mpinzani wake huyo kutoka Afrika Kusini na kutetea mkanda wake.

Alisema anafuatilia rekodi na michezo ya mpinzani wake ili kuhakikisha anafanikiwa kutetea mkanda huo wa ubingwa wa Afrika.

"Naendelea na mazoezi na niko tayari kupambana na mpinzani wangu, natambua ni bondia mzuri na ninaimani kwa maandalizi ninayofanya nitashinda kwa kumpiga mapema Sabelo," alisema bondia huyo.

Promota wa pambano hilo, Saadah Salum, alisema litakwenda sambamba na mpambano kati ya Seleman Kidunda na Patrick Mukala ambalo litakuwa pambano kuu (Main Card).

Alisema pambano hilo walilokuwa nalo awali, wameamua kuliongeza na hilo la Tony ambaye atakuwa na kazi ya kutetea mkanda wake wa ubingwa wa ABU dhidi ya Sabelo kutoka Afrika Kusini, hivyo siku hiyo kupigwa mapambano mawili ya ubingwa wa ABU.

"Maandalizi ukweli yanaendelea vizuri, ingawa wito wetu bado upo kwa wadhamini kuendelea kujitokeza kwa sababu hili ni pambano kubwa kuwahi kutokea katika historia ya Tanzania kutokana na mabondia wawili wa Tanzania kuwania mikanda ya ubingwa wa Afrika ABU ambayo ndiyo mkanda mkubwa wa ubingwa kwa Afrika," alisema Salum.

**UMEFUNIKA...**




Mkuu wa Uhusiano na Mawasiliano wa Benki ya NBC, Godwin Semunyu (kulia), akikabidhi mfano wa hundi yenye thamani ya shilingi milioni moja kwa mchezaji wa Singida Big Stars, Bruno Gomes, baada ya kutangazwa Mchezaji Bora wa Ligi Kuu Bara (NBC Premier League) kwa mwezi Januari 2023, tukio hilo lilifanyika muda mfupi kabla ya kuanza kwa mchezo kati ya Simba na timu yake katika Uwanja wa Benjamini Mkapa, Dar es Salaam Ijumaa iliyopita. Mchezo huo ulimalizika kwa Simba kuibuka na ushindi wa mabao 3-1. **MPIGAPICHA WETU**

# Manula, Diarra wachuana kukaa langoni

**Na Adam Fungamwango**

GOLIKIPA wa Simba, Aishi Manula anaongoza kwa kukaa langoni mechi nyingi za Ligi Kuu Tanzania Bara, huku kipa wa Prisons, Hussein Abel, akiongoza kwa kuokoa michomo mingi langoni mwake maarufu kama 'saves.'

Kwa mujibu wa takwimu za Ligi Kuu baada ya raundi ya 22, Manula amekaa langoni mechi 21, ikiwa ni mara nyingi zaidi kuliko kipa yeyote yule. Kwa maana hiyo hajacheza mechi moja tu ya Ligi Kuu.

Wakati Manula akikaa langoni mara 20, kipa Abel wa Prisons, ambaye alihamia KMC kwenye kipindi cha dirisha dogo la Januari, ameongoza kwa kufanya 'saves' 42 zikiwa ni nyingi zaidi kuliko kipa yeyote.

Ukiachana na Manula, makipa wengine waliosimama langoni mara nyingi ni Djigui Diarra wa Yanga akicheza mechi 19, akiwa hajakaa langoni kwenye mechi tatu za timu yake ya Yanga, huku ikiwa ni pungufu ya mechi mbili kwa anayeongoza.

Diarra anafuatiwa na Said Kipao wa Kagera Sugar ambaye amedaka mechi 18.

Mahmoud Mroivil wa Coastal Union na David Kissu wa KMC wakiwa wamesimama langoni mara 17 na kipa ambaye amecheza mechi chache kwenye Ligi Kuu ni Christopha Masapta wa Polisi Tanzania aliyesimama mara nane tu.

Kwa mujibu wa takwimu hizo ni kwamba, Kissu wa KMC anakamata nafasi ya pili kwa kufanya 'saves' baada ya Abel, kwani ameokoa michomo mara 36, akizidiwa sita tu na anayeongoza.

Lameck Kanyonga, kipa wa Mbeya City, anakamata nafasi ya tatu kwa 'saves' akiwa nazo 26, Hussein Masalanga wa Ruvu Shooting ambaye kwa sasa amehamia Ihefu kwenye dirisha dogo pamoja na Razack Shekimweli wa Mtibwa Sugar, kila mmoja ana 'saves' 25.

## TASWA yapata viongozi wapya

**Na Shufaa Lyimo**

Chama cha Waandishi wa Habari za Michezo nchini (Taswa), kimepata viongozi wapya katika uchaguzi mkuu wao uliofanyika jijini Dar es Salaam jana, ambapo Amiri Mhando amechaguliwa kuwa mwenyekiti kwa kura 57 alizopigiwa na wajumbe wa mkutano mkuu wasiozidi 68.

Akitangaza matokeo ya uchaguzi huo kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi, Milinde Mahona, alisema ameshukuru zoezi hilo limekwenda vizuri bila ya kuwapo kwa malalamiko yoyote.

"Ninashukuru zoezi letu la uchaguzi limemalizika salama wagombea wamepata ushindi kihalali," alisema Mahona.

Kwa upande wa nafasi ya Katibu Mkuu, Mahona alimtangaza Alfred Lucas kushinda kwa kura 57 huku mshindi wa nafasi ya Katibu Mkuu Msaidizi, Imani Makongoro, akiweka rekodi kwa kupata kura zote 68 za wajumbe.

Dina Ismail alitangazwa kuibuka kidedea katika nafasi ya mweka hazina baada ya kupata 65 huku mwenyekiti huyo pia alimtangaza Timzoo Kalugira kushinda nafasi ya ujumbe kwa kura 62 dhidi ya kura 60 za mpinzani wake, Nasongeli Kilinda.

Aidha, baada ya kutangazwa kuwa Mwenyekiti wa Taswa, Mhando kwa niaba ya viongozi wenzake, alisema watashirikiana kufanya kazi pamoja na waandishi wa habari na kuwataka wavunje makundi ya uchaguzi lengo likiwa ni kukiendeleza chama hicho.

"Kwa wale wagombea wenzangu ambao hamjapata kura, msikate tamaa ninaahidi kushirikiana na nyie muda na wakati wowote," alisema Mhando.

Alisema lengo lake ni kukifikisha mbali chama hicho pamoja na kuwataka waandishi wa habari za michezo kubadilika katika uandishi wao.

Naye Ofisa Michezo wa Baraza la Michezo Tanzania (BMT), ambaye pia ni mlezi wa chama hicho, Charles Maguzo, aliwataka viongozi hao kufanya kazi kwa ushirikiano ikiwa ni pamoja na kutafuta ofisi yenye hadhi.

Alisema wahakikishewanapata kadi za wanachama pamoja na kurekebisha katiba yao.

"Waandishi wa habari ni kioo cha jamii, mnapaswa kuandika habari za michezo ambazo zinakuwa zenye ubora na zitakazovutia watu wengi," alisema Maguzo.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MAGUIRE KUONDOKA UNITED

MLINZI wa kati wa England, Harry Maguire, mwenye umri wa miaka 29, na kiungo wa kati wa Scotland, Scott McTominay (26), wataongoza uhamisho wa wachezaji sita wenye majina makubwa Manchester United msimu huu. ***(The Mirror)***

### RICE ATAJWA ARSENAL

KLABU ya West Ham ina uhakika wa kupata ada ya uhamisho wa zaidi ya pauni milioni 80 kwa kiungo wa kati wa England, Declan Rice, huku Newcastle ikitarajiwa kuungana na Arsenal na Chelsea katika mbio za kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24. ***(Football Insider)***

### AUBAMEYANG ASAKWA

KLABU za Barcelona, Atletico Madrid na AC Milan, zote zimefanya uchunguzi kuhusu mshambuliaji wa Gabon, Pierre-Emerick Aubameyang, mwenye miaka 33 baada ya kukosekana kwenye kikosi cha Chelsea cha Ligi ya Mabingwa Ulaya. ***(Mail)***

### OSIMHEN AGOMBEWA

KLABU ya Chelsea iko tayari kupambana na Manchester United kumnunua mshambuliaji wa Napoli na Nigeria, Victor Osimhen, 24. ***(Mirror)***

### BUENO ATAKIWA MADRID

REAL Madrid imeweka nia yao ya kumsaini mlinzi wa Wolverhampton Wanderers na Hispania, Hugo Bueno, 20. ***(AS via Sport Witness)***

### FATI AWANIWA SPURS

KLABU za Arsenal na Tottenham ni miongoni mwa klabu ambazo zimeonyesha nia ya kumnunua mshambuliaji wa Barcelona, Ansu Fati, lakini Bayern Munich wanatajwa kumtaka zaidi mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20. ***(Mundo Deportivo)***

### TIELEMANS HUYOOO ARSENAL

ARSENAL itakuwa inapewa nafasi kubwa ya kumsajili kiungo wa kati wa Leicester City na Ubelgiji, Youri Tielemans mwenye umri wa miaka 25, msimu wa majira ya joto. ***(TeamTalk)***

### SPURS YATAKA NYOTA

KLABU ya Tottenham Hotspur inaweza kuripotiwa kutumia uhusiano mzuri na Atletico Madrid kuwasajili winga wa Ubelgiji, Yannick Carrasco mwenye miaka 29 na kipa wa Slovenia, Jan Oblak (30), katika dirisha lijalo la usajili. ***(Mail)***

### MADRIS WALIMKATAA CANCELO

REAL Madrid walipewa nafasi ya kumsajili beki wa pembeni wa Ureno, Joao Cancelo mwenye miaka 28, kutoka Manchester City, lakini klabu hiyo ya Hispania iliamua kutoendelea na mpango huo kwa vile wanafuraha na kikosi cha sasa. ***(Fabrizio Romano)***

### ISCO NA KLABU MPYA

KIUNGO wa kati wa Hispania, Isco mwenye miaka 30, ameripotiwa kusubiri pendekezo madhubuti kwa wakala wake kutoka Everton huku akiendelea kutafuta klabu mpya baada ya mkataba wake na Sevilla kuvunjwa. ***(TuttoJuve)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# GALTIER AKUNWA KIWANGO KIKUBWA CHA MESSI PSG

**Tuliweza kutokana na ubora wa Leo na dhamira yake, kuipeleka timu kwenye ushindi na kushinda...**

**PARIS, Ufaransa**

KOCHA Christophe Galtier alisifu mchango mwingine wa kushinda mechi kutoka kwa Lionel Messi baada ya Paris Saint-Germain kuifunga Toulouse 2-1 na kuwa mbele kwa pointi nane kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1.

PSG ilipata pigo la mapema kwenye Uwanja wa Parc des Princes Jumamosi wakati kiungo Renato Sanches alipoondoka uwanjani akilia baada ya kujiunga na orodha ya majeruhi inayojumuisha Kylian Mbappe, Neymar na Sergio Ramos.

Mambo yalichukua mkondo mwingine wakati mpira wa adhabu wa Branco van den Boomen ulipoipa Toulouse bao la kuongoza kwa kushtukiza dakika ya 20.

Achraf Hakimi alisawazisha kwa shuti la mguu wa kushoto kutoka umbali wa yadi 20 baada ya kupenya kutoka upande wa kulia dakika saba kabla ya mapumziko.

Hakimi kisha akatoa pasi kwa Messi, ambaye alifunga bao la kwanza kutoka nje ya eneo la hatari na kuongeza uongozi wa PSG dhidi ya Marseille - ambao jana Jumapili walikuwa wanacheza na Nice.

Messi amefikisha mabao 10 kwa msimu huu ikiwa ni msimu wake wa kwanza kufikisha idadi hiyo ya mabao kwa wababe hao wa Paris.

Kocha Mkuu wa PSG, Galtier alifurahishwa na jinsi timu yake ilivyopona baada ya kumpoteza kiungo Sanches. Alisema: "Tulikuwa na mwanzo mgumu wa mechi kutokana na jeraha la Renato mapema. Niliamua kumleta El Chadaille (Bitshiabu) haraka sana, amekuwa akionyesha kwa wiki nyingi kwamba yuko katika kiwango cha Ligue 1.

"Tulifahamu ubora wa Toulouse ni moja ya timu hatari katika Ligue 1 kutoka sehemu ndogo. Lakini kwa ujumla tulidhibiti mchezo. Ilibidi turudi kwenye viwango vya usawa na kuchukua tahadhari dhidi ya safu ngumu ya ulinzi.

"Kwa maana hiyo, Achraf, kama alivyofanya dhidi ya Montpellier ingawa bao lilikataliwa, safari hii alifunga kwa mguu wake wa kushoto.

"Tuliweza, kutokana na ubora wa Leo na dhamira yake, kuipeleka timu kwenye ushindi na kushinda katika mchezo ambao ulionekana kana kwamba tulipaswa kushinda."

SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI

POLISI TANZANIA
VERSUS
KAGERA SUGAR

1 | 2.50
X | 2.55
2 | 2.80

PIGA *150*87#

Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# POTTER SASA AMTULIZA AUBAMEYANG CHELSEA



**LONDON, England**

KOCHA Mkuu wa Chelsea, Graham Potter, amesisitiza kuwa Pierre-Emerick Aubameyang bado ana mustakabali ndani ya Chelsea licha ya uamuzi mgumu wa kumwondoa kwenye kikosi cha Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Potter alimwacha Aubameyang nje ya kikosi chake cha wachezaji 25 kuelekea Ligi ya Mabingwa Ulaya, na kuwaleta wachezaji wapya Joao Felix, Enzo Fernandez na Mykhailo Mudryk.

Mchezaji huyo wa Kimataifa wa Gabon aliichezea Chelsea kwa mara ya mwisho Novemba na amefunga mabao matatu pekee katika mechi 18 ambapo mabao 10 pekee kati ya hayo ndiyo ameanza huku kukiwa na hali ya kutatanisha huko Stamford Bridge.

Lakini Aubameyang alifunga mabao mawili nyumbani na ugenini dhidi ya AC Milan kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, akianza mechi zote sita, huku Potter akikiri ugumu wa kutaja kikosi chake na utajiri wa Chelsea.

Potter alisema: "Sidhani itakuwa ngumu kwa sababu Pierre ni mtaalamu na bila shaka, ninaelewa kuwa hatakatishwa tamaa. Ulikuwa uamuzi mgumu. Tulikuwa na watatu ndani na wawili walipaswa kutoka. Yeye ndiye aliyekosa, hakuna kosa lolote alilofanya."

Picha iliyowekwa kwenye Instagram na kaka yake Aubameyang, Willy ilizua utata baada ya kuonekana kuwa mshambuliaji huyo wa zamani wa Arsenal alikuwa nchini Italia huku Chelsea ikilazimishwa sare na Fulham Jumamosi.

Potter aliondoa uvumi juu ya kutokuwapo kusikotarajiwa, ingawa, alielezea kuwa Aubameyang alikuwa huru kufanya anachotaka na nafasi adimu ya kuchukua muda, huku akisema kuwa alifanya mazoezi na amefanya vizuri sana hivyo atapata mapumziko wikendi ili aripoti leo Jumatatu.

# Greenwood kutimkia China

**MANCHESTER, England**

MASON Greenwood inaripotiwa kuwa yuko tayari kufufua maisha yake ya soka nchini China iwapo Manchester United itavunja mkataba wake.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 21, sasa yuko chini ya uchunguzi wa ndani wa klabu iwapo ataingia tena kwenye kikosi cha kwanza cha kocha Erik ten Hag.

Hali hii inakuja baada ya mashtaka ya madai ya ubakaji na shambulio dhidi ya Greenwood kutupiliwa mbali na waendesha mashtaka wiki hii.

Kwa mujibu wa gazeti la The Sun, Greenwood amekubali kwa huzuni mchakato wa ndani wa United ambao unatoa muda wa kufanya uamuzi kuhusu mustakabali wake.

Gazeti hilo limedai kwamba Greenwood alipofungiwa na United mwaka jana, muda mfupi baada ya kukamatwa Januari, aliapa kutoichezea klabu hiyo tena.

Chanzo kimoja kilisema: "Wakati huo alikuwa akisisitiza kwamba hataki kuvaa jezi nyekundu tena, alihisi kama klabu haikuwa upande wake.

"Alisema atafurahi kwenda kucheza China mradi tu analipwa vizuri na anacheza."

"Mtazamo wake unaweza kuwa kweli katika miezi michache iliyopita, lakini hakuwa na furaha hata kidogo."

Wengine waliliambia gazeti la The Sun kuwa wanahofia Greenwood angekabiliana na wimbi la unyanyasaji ambao bila shaka angekabiliana nalo kutoka kwa mashabiki wapinzani iwapo atarejea kwenye Ligi Kuu.



CHEZA USHINDE KASINO
JISAJILI
CHEZA
SHINDA

# LUKULA AKUNWA USAJILI WA GAUCHO SIMBA QUEENS

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa timu ya soka ya Wanawake ya Simba Queens, Charles Lukula, amefunguka kuwa usajili wa Mwanahamisi Omari maarufu Gaucho, aliyesajiliwa kipindi cha dirisha dogo, umeleta uhai mkubwa kwenye kikosi hicho kwa sasa.

Akizungumza na gazeti hili kuhusu maendeleo ya kikosi cha timu hiyo ambacho kwa sasa kinapigana kuutetea ubingwa wake, amesema Gaucho amesababisha timu iwe na uhai, ikionekana kuwa tishio kwa timu pinzani kutokana na uwezo mkubwa aliokuwa nao.

"Kwa sasa nina furaha sana kwa sababu hata kama mchezaji fulani hayupo huna wasiwasi, waliobaki wanaweza kucheza na hii ilitokana na wachezaji wangu kucheza mechi nyingi sana mfululizo msimu uliopita, Ligi Kuu, CECAFA, wengine walikwenda Morocco kwenye Kombe la Dunia ya vijana, halafu Ligi ya Mabingwa Afrika, kusema kweli walichoka, hii ikanifanya nianze kuwapumzisha baadhi kuwachezesha wengine, lakini sasa wameanza kurudi kwenye hali ya kawaida, ndiyo maana tumeanza kufunga mabao mengi.

"Kingine ni usajili wa Mwanahamisi Gaucho, umeleta kitu, umeleta uhai mkubwa ndani ya kikosi chetu. Uwapo wake ni muhimu kwani ana uwezo mkubwa, halafu amekuja kipindi ambacho wachezaji wameanza kurudi kwenye viwango vyao na kama ikiendelea hivi, tunaweza kabisa kuutetea ubingwa," alisema kocha huyo ambaye timu yake inashika nafasi pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya Wanawake nchini nyuma ya JKT Queens.



Kocha Mkuu wa timu ya soka ya Wanawake ya Simba Queens, Charles Lukula

Gaucho ambaye alikuwa nahodha wa kikosi hicho, alisajiliwa nchini Morocco mwaka 2021 kwenye klabu ya Chabab Atlas inayocheza Ligi Kuu, lakini kwa sasa amerejea tena kikosini.

Kuhusu kutoonekana kwa Fatuma Issa 'Fetty Densa' kwenye michezo mbalimbali, lakini Opa Clement kwenye mechi dhidi ya Alliance Girls, alisema wachezaji hao wote ni majeruhi.

"Fetty Densa yeye kwa sasa amepona, anatafuta tu utimamu wa mwili ili arejee uwanjani, Opa aliumia kwenye mechi yetu dhidi ya Amani Queens huko Lindi, madaktari wamemwambia apumzike kwa wiki moja, baada ya hapo wote mtawaona uwanjani," alisema kocha huyo raia wa Kenya.

# SIMBA, AL HILAL KUMENOGA CAF

INATOKA UK. 24

Simba, kwani kuingia kwa wachezaji wake tegemeo, Clatous Chama, Mzamiru Yassin, Shomari Kapombe, Mohamed Hussein 'Tshabalala' na Pape Sakho yaliifanya timu hiyo kubadilika na kusukuma mashambilizi makali langoni mwa wageni wao.

Alikuwa ni Habib Kyombo aliyeisawazishia Simba bao dakika tisa kabla ya mechi kumalizika, lililotokana na kazi kubwa iliyofanywa na Bocco, aliyemmegea pande Sakho, akiwa kwenye wingi ya kushoto akawahadaa walinzi wa Al Hilal na kupiga krosi iliyomkuta mfungaji ambaye alitulia kabla ya kuachia shuti lililogonga nguzo ya kulia kwa kipa Ashrem na kutinga upande wa kushoto.

Beno Kakolanya alifanya kazi ya ziada kwa kuokoa mabao mawili ya wazi dakika ya 73 na 74 akiwa anatazamana na mastraika John Otenyai na dakika moja baadaye Yasir Mozamir, lakini aliruka na kupangua michomo hiyo kwa ustadi mkubwa.

Baada ya mchezo huo, Kocha Florent Ibenge wa Al Hilal, alisema ameridhishwa na kipimo hicho kwani alikuwa na wachezaji wote kwenye mechi hiyo, na kila mmoja alitaka kumuonyesha yupo tayari kiasi gani kwa ajili ya mechi za makundi Ligi ya Mabingwa Afrika.

# NABI AFUNGUKA MCHEZO MBAYA

INATOKA UK. 24

kwanza hawakucheza vizuri na kuruhusu kufungwa mabao mepesi kwa sababu ya kufanya makosa.

Alisema wachezaji hawakuwa makini baada ya mchezaji mmoja kuumia na walishindwa kujipanga kwa haraka na kuruhusu kufungwa bao rahisi.

"Kipindi cha pili tulicheza vizuri, tumeyapokea matokeo hayo tunarejea uwanjani kufanyia kazi mapungufu yetu na kujipanga kwa mechi zijazo ili kufikia malengo yetu ya kutaka kumaliza ligi katika nafasi nzuri," alisema Kitambi.

SPORTPESA APP
PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI
"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATATU - 06/02/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:00 | 3351 | Egnatia Rrogozhine vs KF Tirana | 3.42 | 3.16 | 2.04 |
| 15:15 | 2727 | AL Ahed vs Shabab Al Ghazieh | 1.13 | 6.04 | 18.74 |
| 15:25 | 5241 | AL Sahel SC vs AL Arabi (SA) | 3.48 | 2.96 | 2.11 |
| 15:50 | 2461 | AL Qaisoma vs AL Ain | 2.24 | 2.80 | 3.00 |
| 16:00 | 4422 | Polisi Tanzania vs Kagera Sugar | 2.50 | 2.55 | 2.80 |
| 16:15 | 1086 | Hatta Club vs Emirates Club | 2.31 | 3.15 | 2.55 |
| 16:15 | 5588 | Masfoot Sports Club vs Al-Hamriyah | 3.40 | 3.35 | 1.83 |
| 16:20 | 4689 | City Football Club vs Ahli Al-Fujirah | 5.19 | 3.89 | 1.54 |
| 17:00 | 1312 | Sabah vs Sabayil | 1.33 | 4.65 | 7.44 |
| 17:00 | 2348 | Sochi vs Rostov | 2.85 | 3.37 | 2.21 |
| 17:00 | 2356 | Umraniyespor vs Adana Demirspor | 3.19 | 3.66 | 2.05 |
| 17:00 | 4000 | Levadiakos vs Volos | 2.37 | 3.12 | 3.01 |
| 17:00 | 4175 | Delhi Dynamos FC vs FC Goa | 2.90 | 3.48 | 2.14 |
| 18:00 | 2716 | Botosani vs Petrolul Ploiesti | 2.11 | 3.17 | 3.43 |
| 18:00 | 4651 | Farco FC vs Zamalek | 4.86 | 3.03 | 1.86 |
| 19:00 | 4885 | Asi D Abengourou vs Denguele Sport | 2.80 | 2.69 | 2.69 |
| 20:00 | 1368 | Hapoel Petah Tikva vs Nazareth Ilit | 1.74 | 3.67 | 4.47 |
| 20:00 | 2882 | Hapoel Afula vs Ironi Tiberias | 3.10 | 3.21 | 2.30 |
| 20:00 | 3861 | Eyupspor vs Bodrumspor | 1.89 | 3.32 | 3.73 |
| 20:00 | 3983 | FC Krasnodar vs Spartak Moscow | 2.95 | 3.52 | 2.09 |
| 20:00 | 5450 | Fenerbahce vs Konyaspor | 1.47 | 4.33 | 6.13 |
| 20:00 | 5759 | Aris Limassol vs Doxa Katokopia | 1.39 | 4.58 | 7.45 |
| 20:00 | 5845 | Giresunspor vs Kayserispor | 2.46 | 3.28 | 2.75 |
| 20:05 | 4902 | Jeddah Club vs Alshoulla | 1.96 | 2.85 | 3.60 |
| 20:30 | 1963 | Verona vs Lazio | 3.62 | 3.33 | 1.99 |
| 21:00 | 1597 | Waldhof Mannheim vs Verl | 1.96 | 3.44 | 3.60 |
| 21:00 | 2778 | CD Feirense vs Covilha | 1.74 | 3.53 | 4.42 |
| 21:00 | 3692 | Farul Constanta vs Universitatea Craiova | 2.64 | 3.02 | 2.70 |
| 21:00 | 4114 | Korona Kielce vs Cracovia | 3.11 | 3.16 | 2.17 |
| 21:00 | 4172 | Diosgyori Vtk vs Duna Aszfalt Tvse | 1.30 | 4.65 | 8.48 |
| 21:00 | 5197 | Lommel U21 vs St Truiden U21 | 4.56 | 4.36 | 1.54 |
| 21:00 | 5446 | Sport Boys Association vs Union Comercio | 2.05 | 3.32 | 3.21 |
| 21:30 | 1150 | Hapoel Hadera vs Maccabi Haifa | 7.66 | 4.66 | 1.32 |
| 21:30 | 1395 | Portuguesa RJ vs Volta Redonda RJ | 2.90 | 2.90 | 2.44 |
| 21:30 | 5289 | Kortrijk U21 vs RWD Molenbeek U21 | 2.06 | 3.20 | 2.90 |
| 22:00 | 1363 | Jong Ajax vs PEC Zwolle | 4.41 | 4.41 | 1.58 |
| 22:00 | 3068 | Real Santa Cruz vs Club Atletico Palmaflor | 2.33 | 3.52 | 2.59 |
| 22:00 | 4745 | Willem II Tilburg vs FC Eindhoven | 2.25 | 2.90 | 2.85 |
| 22:00 | 4763 | Portimonense vs Pacos Ferreira | 2.02 | 3.17 | 3.77 |
| 22:00 | 5034 | Lierse SK U21 vs Oostende U21 | 5.40 | 4.40 | 1.38 |
| 22:00 | 5375 | Kmsk Deinze U21 vs Westerlo U21 | 4.57 | 4.26 | 1.55 |
| 22:30 | 4276 | Avellino vs Crotone | 3.26 | 2.88 | 2.40 |
| 22:45 | 2343 | Amiens vs Metz | 2.49 | 3.13 | 2.79 |
| 22:45 | 4974 | Monza vs Sampdoria | 1.75 | 3.42 | 4.66 |
| 23:00 | 2904 | Burgos vs Las Palmas UD | 3.77 | 3.03 | 2.06 |
| 23:00 | 3127 | Blackburn vs Wigan | 1.97 | 3.31 | 3.71 |
| 23:00 | 3139 | Venezuela U20 vs Uruguay U20 | 6.65 | 3.89 | 1.44 |
| 23:00 | 3182 | Rayo Vallecano vs Almeria | 1.79 | 3.54 | 4.39 |
| 23:00 | 3491 | Le Mans vs Concarneau | 2.46 | 3.20 | 2.73 |
| 23:30 | 3149 | Cesar Vallejo vs Alianza Atletico | 1.69 | 3.58 | 4.36 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumatatu Februari 6, 2023


Nipashe




UKURASA 21

**Galtier akunwa kiwango kikubwa cha Messi PSG**

**HAMNIWEZI...**




Pape Sakho akimiliki mpira dhidi ya wachezaji wa Al Hilal huku Shomari Kapombe (kushoto), akiwahi kuomba pasi kwenye mechi ya kimataifa ya kirafiki iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa jana na kumalizika kwa sare ya bao 1-1. **MPIGAPICHA WETU**

# SIMBA, AL HILAL KUMENOGA CAF

## Zapata kipimo sahihi cha kuzivaa Horoya na Mamelodi Sundowns, Ibenge asema...

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba na Al Hilal ya Sudan, zimeonyeshana mwanga wa mechi za hatua ya makundi kuelekea michezo yao ya mwishoni mwa wiki hii zitakapokuwa ugenini nchini Guinea na Afrika Kusini kuanza kusaka tiketi ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Simba ambayo Jumamosi itakuwa nchini Guinea kucheza dhidi ya Horoya AC, huku Al Hilal ikiwa Afrika Kusini kukipiga dhidi ya Mamelodi Sundowns, zilitoka sare ya bao 1-1 jana katika mchezo wa kirafiki wa kimataifa uliopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Ilikuwa ni mechi kali ambayo kila timu ilikuwa ikionyesha ni nini itakwenda kukionyesha kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya makundi.

Iliwachukua dakika sita tu kwa wageni, Al Hilal kupata bao la kuongoza dhidi ya Simba ambayo ilianzisha wachezaji wawili tu wa kikosi chake cha kwanza, Henock Inonga na Jean Baleke, shukrani zikimwendea mchezaji wa Kimataifa wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Makabi Lilepo, aliyewatanguliza Wasudan hao.

Lilepo alifunga bao hilo kutokana na faulo iliyopigwa na Ahmed Yahaya, baada ya Ismael Sawadogo kumfanyia madhambi David Abagra.

Baada ya bao hilo, Simba ilionekana kuamka kwenye usingizi mzito, kwani ilianza kufanya mashambulizi na dakika moja baadaye ilikosa bao kupitia kwa Baleke ambaye alipiga kichwa kilichopaa juu, akiunganisha krosi ya Gadiel Michael.

Hata hivyo, straika huyo aliyesajiliwa kipindi cha dirisha dogo la usajili Januari mwaka huu, alitolewa nje ya uwanja baada ya kuumia katikati ya kipindi cha kwanza na nafasi yake kuchukuliwa na nahodha John Bocco.

Timu hizo ziliendelea kumiliki mpira kwa zamu, lakini ilikuwa ni Simba iliyoshindwa kutumia nafasi mbili ambazo zingeweza kuipeleka hadi mapumziko ikiwa inaongoza.

Kibu Denis alijitengea mpira mwenyewe dakika ya 14 na kuachia shuti kali ambalo halikulenga lango, mpira ukapiga pembeni kidogo ya lango.

Sekunde chache kabla ya mapumziko, Sawadogo akiwa nje ya eneo la hatari, naye alipiga shuti kali ambalo halikulenga lango vizuri, lakini kipa Ali Abo Ashren alikuwa ameshakubali akiuangalia mpira ulikokuwa unaelekea.

Kipindi cha pili timu zote zilifanya mabadiliko ambayo yalitoa faida zaidi kwa

INAENDELEA UK. 23

## Nabi afunguka mchezo mbaya Yanga, Namungo

**Na Saada Akida**

BAADA ya kushindwa kuonyesha soka la kuvutia katika ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Namungo FC juzi, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amesema sababu hasa ni mpango mkakati wa mechi ya Kombe la Shirikisho Afrika iliyo mbele yao.

Katika mchezo huo uliopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi, Nabi aliwapa nafasi Salum Abubakari 'Sure Boy', Khalid Aucho na Stephen Aziz Ki, ambao walirejea uwanjani baada ya kupona majeruhi waliyoyapata katika michezo ya nyuma.

Jumapili wiki hii Yanga itashuka dimbani ugenini nchini Tunisia dhidi ya US Monastir, huo ukiwa mchezo wao wa kwanza wa hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Akizungumza na Nipashe jana, Nabi alisema aliwapa nafasi ya kucheza wachezaji hao waliopona majeraha yao hivi karibuni, ili kuwajenga kuwa fiti na tayari kwa kucheza mechi ya ushindani ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya US Monastir ya Tunisia.

Nabi alisema anashukuru kupata pointi tatu, licha ya kwamba hawakucheza katika ubora wao kama ilivyo kwa mechi za nyuma walizocheza.

Alisema anatambua kwa nini hawakucheza vizuri katika mchezo huo na kwamba kubwa zaidi ni kwa sababu ya kuwapa nafasi wachezaji waliotokea chumba cha majeruhi, na kwamba lengo lake la kuwajenga na kuwa tayari kwa mchezo ujao wa CAF lilitimia vema.

"Tumepata ushindi katika mchezo mgumu, lakini hatukucheza vizuri. Tunashukuru tumepata matokeo na hilo la kucheza vibaya nafahamu ni kwa sababu ipo hivyo na tutaenda kufanyia kazi hilo.

"Niliwapa nafasi nyota hao watatu kwa sababu ya kuwaandaa kwa ajili ya mechi ijayo ya kimataifa ambayo itakuwa ya ushindani na tunatakiwa kwenda tukiwa fiti kwa ajili ya kusaka matokeo mazuri katika michuano ya kimataifa," alisema Nabi.

Naye Kocha Mkuu Namungo FC, Denis Kitambi, alisema kipindi cha

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >